# Smart E8
## Mwongozo wa Mtumiaji



VFD 512

# Kuhusu mwongozo huu

Asante kwa kuchagua kifaa hiki cha mkononi. Ili udumishe kifaa chako katika hali yake nzuri, tafadhali soma mwongozo huu na uuweke kama kumbukumbu ya baadaye.

## Hakimiliki


**Hakimiliki © 2017 ZTE CORPORATION**

**Haki zote zimehifadhiwa.**

Hakuna sehemu yoyote ya uchapishaji huu inaweza kunukiliwa, kunakiliwa, kufasiriwa au kutumiwa kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ile, ile kielektroniki au kiufundi, ikiwa ni pamoja na kunakili na filamu ndogo, bila ruhusa iliyoandikwa kbala ya ZTE Corporation.


## Notisi

ZTE Corporation inahifadhi haki ya kufanya marekebisho kwenye hitilafu za maandishi au kusasisha vipimo katika mwongozo huu bila notisi ya kabla. Mwongozo huu umeundwa kwa umakinifu wa juu ili kuhakikisha usahihi wa maudhui haya. Hata hivyo, taarifa zote, maelezo na mapendekezo yote yaliyo hapa ndani hayajumuishi waranti ya aina yoyote, iliyoelezwa au kudhaniwa.

## Kanusho

ZTE Corporation inakanusha kwa uwazi wajibu wowote kwa kasoro na uharibifu unaosababishwa na marekebisho ya programu yasiyoidhinishwa.

Picha na vielelezo-skrini vilivyotumiwa katika mwongozo huu huenda vikatofautiana na bidhaa halisi. Maudhui ya mwongozo huu huenda yakatofautiana na bidhaa au programu halisi.

## Alama za biashara

ZTE na nembo za ZTE ni alama za biashara za ZTE Corporation.

Google Na Android ni alama za biashara za Google, Inc.

Alama za biashara na nembo za Bluetooth® zinamilikiwa na Bluetooth SIG, Inc. Na matumizi yoyote ya alama kama hizi za biashara na ZTE Corporation yanaruhusiwa na leseni.

Nembo ya microSDXC ni alama ya biashara ya SD-3C, LLC.

Vichakataji vya Qualcomm® Snapdragon™ ni bidhaa za Qualcomm Technologies, Inc.

Qualcomm na Snapdragon ni alama za biashara za Qualcomm Incorporated, zilizosajiliwa nchini Marekani na nchi zingine. Imetumiwa kwa idhini.

Alama zingine za biashara na majina mengine ya biashara ni mali ya wamili husika.

**Na. ya Toleo:** R1.0

**Muda wa Toleo:** Tarehe 7 Julai, 2017

# Yaliyomo


**Kuanza ........................................................ 7**

Kuielewa simu yako ........................................ 7

Kujua vibonye ................................................ 8

Kusanidi Simu Yako ........................................ 8

Kuchaji betri ................................................. 11

Kurefusha maisha ya betri ............................. 12

Kuwasha/kuzima ............................................ 13

Kusanidi kwa mara ya kwanza ........................ 13

Kufunga/kufungua simu na vibonye ............... 13

Kutumia skrini ya mguso ................................. 14

Kujua kuhusu skrini ya mwanzo ...................... 16

**Kujua mambo msingi .................................. 18**

Kufuatilia hali ya simu .................................... 18

Kudhibiti taarifa ............................................. 19

Kuingiza maandishi ........................................ 20

Kuhariri maandishi ......................................... 20

Kufungua na kubadilisha programu ................ 21

Tumia programu mbili katika modi ya skrini iliyogawanywa ........................................................ 22

Kusakinusha programu ................................... 22

Kuficha programu ........................................... 23

**Kuunganisha kwenye mitandao na vifaa..... 24**

Kuunganisha kwenye mitandao rununu .......... 24

Kuunganisha kwenye Wi-Fi ............................. 26

Unganisha kwenye kifaa kingine kupitia Wi-Fi Direct® ........................................................ 28

Kuunganisha vifaa vya Bluetooth ................... 28

Kuunganisha kwenye kompyuta yako kupitia USB .. 30

Kutumia kadi ya microSD kama hifadhi ya kubebeka au ya ndani ................................................ 31

Kushiriki muunganisho wako wa data rununu ........... 34


Kuunganisha kwenye mitandao mnemba ya kibinafsi ........................................................ 36

Simu ........ 38
Kupiga na kukata simu ........ 38
Kujibu au kukataa simu ........ 38
Kutumia historia ya simu ........ 39
Kupigia anwani zako simu ........ 40
Anwani ........ 41
Kuangalia maelezo ya anwani ........ 41
Kuongeza anwani mpya ........ 41
Kuunda wasifu wako binafsi ........ 41
Kuingiza, kuhamisha, na kushiriki anwani ........ 42
Kutumia anwani unazozipenda zaidi ........ 43
Kutafuta anwani ........ 44
Kuhariri anwani ........ 44
Akaunti za wavuti ........ 46
Kuongeza au kuondoa akaunti ........ 46
Kusanidi ulandanishaji wa akaunti ........ 46
Barua pepe ........ 48
Kuunda akaunti ya kwanza ya barua pepe ........ 48
Kuangalia barua pepe ........ 48
Kujibu simu ........ 48
Kuandika na kutuma barua pepe ........ 49
Kuongeza na kuhariri akaunti za barua pepe ........ 50
Kubadilisha mipangilio ya jumla ya barua pepe ........ 51
Ujumbe ........ 52
Kufungua skrini ya ujumbe ........ 52
Kutuma ujumbe ........ 52
Kujibu ujumbe ........ 53
Kusambaza ujumbe ........ 53
Kivinjari wavuti ........ 54
Kufungua kivinjari ........ 54
Kutumia vichupo vingi vya kivinjari ........ 54
Kupakua faili ........ 55
Kubadilisha mipangilio ya Chrome ........ 55

**Kamera ........................................................ 56**
Kupiga picha ........................................................56
Kurekodi video ........................................................57
Kutumia modi ya kamera ya kufanya mwenyewe ....58
**Muziki ........................................................ 59**
Kucheza muziki wako........................................................59
Kudhibiti orodha za kucheza ........................................................61
**Mipangilio........................................................ 63**
Pasi waya na mitandao ........................................................63
Kifaa ........................................................65
Maelezo ya kibinafsi ........................................................69
Mfumo........................................................73
**Usuluhishaji ........................................................ 75**

# Kuanza

## Kuielewa simu yako




| Nambari | Jina |
|---|---|
| 1 | Plagi ya vipokea sauti |
| 2 | Chombo cha kuslikiliza |
| 3 | Kamera ya mbele |
| 4 | Mikrofoni kuu |
| 5 | Plagi ya kuchaji/USB mikro |
| 6 | Kibonye cha nishati |
| 7 | Kibonye cha kiwango-sauti |
| 8 | Taa ya kiashiria |
| 9 | Kamera ya nyuma |
| 10 | Mwako wa nyuma |
| 11 | Kihisio cha ukaribu na mwangaza |
| 12 | Mikrofoni Saidizi |

## Kujua vibonye

| Kibonye | Kazi |
|---|---|
| Kibonye cha nishati | • Bonyeza na ushikilie ili uwashe au uzima modi ya ndege, uwashe upya, uwashe au uzime mtetemeko au sauti, uzime simu, au unase kielelezo-skrini.<br>• Bonyeza ili uzime au uwashe onyesho la skrini. |
| Kibonye cha kiwango-sauti | Bonyeza au ushikilie upande wowote wa mwisho wa kibonye ili uongeze au upunguze kiwango-sauti. |
| Kibonye cha mwanzo | • Gusa ili urudi kwenye skrini ya mwanzo kutoka kwenye programu au skrini yoyote.<br>• Gusa na ushikilie ili utumie Utafutaji wa Google au Now on Tap. |
| Kibonye cha nyuma | Gusa ili urudi kwenye skrini ya awali. |
| Kibonye cha programu za hivi karibuni | Gusa ili uone programu zilizotumiwa hivi karibuni. |


## Kusanidi Simu Yako

Zima simu yako kabla ya kuondoa au kubadilisha betri. Zima simu yako kabla ya kuingiza au kuondoa kadi ndogo ya SIM. Kadi ya microSDXC (ya hiari) inaweza kuingizwa au kuondolewa wakati simu imewashwa, lakini unahitaji kuitenganisha kabla ya kuindoa.

**ONYO!**


Ili uepuke kuharibu simu, usitumie aina yoyote nyingine ya kadi za SIM, au kadi zozote ndogo za SIM zisizotimiza kiwango kianachofaa zilizokatwa kutoka kadi ya SIM. Unaweza kupata kadi ndogo ya SIM kutoka kwa mtoa huduma wako.

1. Ingiza kucha yako ya kidole kwenye sloti ya upande wa chini kushoto wa kifuniko cha nyuma na ukiinue polepole.



2. Ingiza kadi ndogo za SIM na kadi ya microSDXC (ya hiari).


   ► Telezesha kadi ndogo za SIM kwenye sloti za kadi.





**DOKEZO:**

Sloti 1 ya SIM ndogo inakubali mitandao ya 4G/3G/2G, huku sloti 2 ya SIM ndogo inakubali mitandao ya 3G/2G.


- Shikilia kadi ya microSDXC kona ya mkato ikiangalia kama ilivyoonyeshwa na uiingize kwenye sloti ya kadi.



3. Ingiza betri. Hakikisha viunganishi vilivyo kwenye betri vinaingia kwenye sehemu za betri kwanza na vinalingana na viunganishi vilivyo ndani yake. Sukuma betri chini polepole hadi litoshee.



4. Funga kifuniko cha nyuma kwa mpangilio na mwelekeo kama ilivyoonyeshwa katika mchoro.



## Kuchaji betri


Betri la simu yako linafaa kuwa na nishati ya kutosha ili simu yako iwake, ipate wimbi, na kupiga simu. Unafaa kuchaji betri kabisa haraka iwezekanvyo.

Ikiwa nishati ya betri iko chini, kutakuwa na kidukizo cha ujumbe kwenye skrini.

**ONYO!**

Tumia chaja na kebo zilizoidhinishwa peke yake. Kutumia vikorokoro visivyoidhinishwa kunaweza kuharibu simu yako au kusababisha betri kulipuka.

1. Unganisha adapta kwenye plagi ya kuchaji. Hakikisha kwamba adapta imeingizwa kwa mwelekeo sahihi. Usikilazimishe kiunganishi kwenye plagi ya kuchaji.



2. Unganisha chaja kwenye soketi ya kawaida ya nishati ya AC. Ikiwa simu imewashwa, utaona ikoni ya kuchaji, kama vile au , ikionekana kwenye mwambaa wa hali.
3. Tenganisha chaja wakati betri limejaa nishati.

**DOKEZO:**

Ikiwa nishati ya betri iko chini sana, huenda usiweze kuwasha simu hata wakati inachajiwa. Katika hali hii, jaribu tena baada ya kuchaji simu kwa angalau dakika 20. Wasiliana na huduma kwa wateja ikiwa bado huwezi kuwasha simu baada ya kuchaji kwa muda mrefu.

## Kurefusha maisha ya betri

Programu amilifu, viwango vya uangavu wa skrini, matumizi ya Bluetooth na Wi-Fi na vipengele vya GPS vinaweza kumaliza nishati ya betri. Unaweza kufuata vidokezo muhimu vilivyo hapa chini kuhifadhi nishati ya betri lako:

- Tumia kipengele cha kihifadhi betri katika Mipangilio.
- Punguza muda wa mwangaza wa skrini.
- Punguza uangavu wa skrini.
- Zima Wi-Fi, Bluetooth na mlandanisho otomatiki wakati hautumiki.
- Lemaza kipengele cha GPS wakati hakitumiki. Programu nyingi zinazotumia kipengele hiki zitaomba maelezo ya eneoulipo mara kwa mara kutoka kwa setilaiti za GPS, na kila ombi litapunguza nishati ya betri lako.

## Kuwasha/kuzima

- Bonyeza na ushikilie kibonye cha **Nishati** ili uwashe simu yako.
- Kuizima, bonyesha na ushikilie kibonye cha **Nishati** ili ufungue menyu ya chaguo na uguse **Zima**.

## Kusanidi kwa mara ya kwanza

Unapowasha simu yako kwa mara ya kwanza baada ya kuinunua au kuweka mipangilio yake ya kiwanda upya (angalia Akibisha na uweke upya), unahitaji kuweka mipangilio kadhaa kabla ya kuitumia.

Gusa kipengele cha lugha ili uchague lugha. Kisha fuata visituo vilivyo kwenye skrini ili usanidi simu yako.

## Kufunga/kufungua simu na vibonye

Simu yako hukuruhusu kufungua skrini na vibonye haraka (weka simu kwa modi ya kulala) wakati haitumiki na kuwasha skrini tena na kuifungua wakati unaihitaji.

**Kufunga skrini na vibonye:**

Ili uwashe skrini na kufungua vibonye haraka, bonyeza kibonye cha **Nishati**.

**DOKEZO:**

Kuhifadhi nishati ya betri, simu huzima skrini kiotomatiki baada ya muda fulani bila shughuli. Bado utaweza kupokea ujumbe na simu wakati skrini ya simu imezimwa.

**Kufungua skrini na vibonye:**

1. Bonyeza kibonye cha **Nishati** ili uwashe skrini.

   - au -

   Gusa skrini mara mbili ili uiwashe.

   **DOKEZO:**

   Ili uwezeshe kipengele hiki, chagua > **Mipangilio > Onyesho > Gusa mara mbili uamshe** kutoka kwenye skrini ya mwanzo.

2. Telezesha juu kwenye skrini.

   - au -

Telezesha kutoka kwenye ikoni ya mkato iliyo upande wa chini ili ufungue programu au kipengele husika.

- au -

Gusa taarifa mara mbili kwa mfululizo ili ufungue programu husika.

**DOKEZO:**

Unaweza kuhariri ikoni za mkato kwenye skrini ya kufunga. Chagua > **Mipangilio** > **Onyesho** > **Hariri Mikato ya Skrini Iliyofungwa** kutoka kwenye skrini ya mwanzo, gusa mkato ili uubadilishe, au gusa **Ongeza mkato** ili uongeze mmoja.

## Kutumia skrini ya mguso

Skrini ya mguso ya simu yako hukuwezesha kudhibiti hatua kupitia ishara mbalimbali za mguso.

- Gusa

  Unapotaka kucharaza kwa kutumia kibodi iliyo kwenye skrini, chagua vipengele vilivyo kwenye skrini kama vile ikoni za programu na mipangilio, au ubonyeze vitufe vilivyo kwenye skrini, viguse kwa kidole chako.



- Gusa na Ushikilie

  Ili ufungue chaguo zinazopatikana za kipengele (kwa mfano, ujumbe au kiungo katika ukurasa wa tovuti), gusa na uvishikilie.




- Telezesha

  Kutelezesha kunamaanisha kukokota kidole chako wima au mlalo katikati mwa skrini.




- Kokota

  Kukokota, bonyeza na ushikilie kidole chako na nguvu kiasi kabla ya kuanza kusongeza kidole chako. Wakati unakokota, usiinue kidole chako hadi ufikie nafasi lengwa.



- Chuna

  Katika baadhi ya programu (kama vile Ramani na kivinjari wavuti), unaweza kukuza zaidi na kufifiza kwa kuweka vidole viwili kwenny skrini kwa wakati moja na kuvichuna pamoja (ili kufifiza) au kuvipanua (ili kukuza).



- Zungusha skrini

  Kwa skrini nyingi, unaweza kubadilisha mwelekeo wa skrini kiotomatiki kutoka picha wima na kuwa picha mlalo kwa kugeuza simu ilale kibavu.

  **DOKEZO:**

  Kipengele cha ugeuzaji otomatiki kinahitaji kuwezeshwa ili mwelekeo wa skrini ubadilishwe kiotomatiki. Gusa **>** **> Mipangilio > Onyesho > Wakati kifaa kinazungushwa** na uchague **Zungusha maudhui ya skrini**.

  Unaweza pia kufikia udhibiti wa uzungushaji wa skrini kwa kutelezesha mwambaa wa hali chini mara mbili na uguse **Zungusha kiotomatiki/Picha-wima.**

# Kujua kuhusu skrini ya mwanzo

Skrini ya mwanzo ndio sehemu ya kuanza kwa programu, vipengele, na menyu za simu yako. Unaweza kukaidisha skrini yako ya mwanzo kwa kuongeza mikato, folda, wiji, na zaidi.




### Paneli pana za skrini ya mwanzo

Skrini yako ya mwanzo inaweza kupanuliwa, kuongeza nafasi zaidi kwa mikato, wiji, na zaidi. Telezesha kushoto au kulia kwenye skrini ya mwanzo ili uone paneli zilizopanuliwa. Unaweza kuongeza au kuondoa paneli za skrini ya mwanzo, au kusawazisha mipangilio yao.

### Kuongeza paneli mpya ya skrini ya mwanzo:

1. Gusa na ushikilie sehemu tupu ya skrini ya mwanzo ili ufikie vijipicha vya skrini ya mwanzo.
2. Telezesha kushoto hadi + ionekane.
3. Gusa + uunde paneli mpya ya skrini ya mwanzo.

### Kusawazisha mpangilio wa paneli ya skrini ya mwanzo:

1. Gusa na ushikilie sehemu tupu ya skrini ya mwanzo na utelezeshe kushoto au kulia uone vijipicha vya skrini ya mwanzo.
2. Gusa na ushikilie kijipicha na ukikokote kushoto au kulia hadi sehemu unakihitaji.

**Kufungua programu unayoipenda zaidi ya skrini ya mwanzo:**

Unaweza kutelezesha kulia kwenye skrini ya mwanzo ili ufungue programu unayoipenda zaidi haraka.

1. Telezesha kulia kwenye skrini ya mwanzo ikiwa inahitajika ili ufikie skrini ya mwanzo iliyo kushoto zaidi.
2. Telezesha kulia kwenye skrini ili ufungue programu unayoipenda zaidi.

**DOKEZO:**

Gusa > > **Mipangilio > Onyesho > Paneli ya programu unayoipenda zaidi** uwashe au uzime kipengele hiki, au gusa **Programu unayoipenda zaidi ya skrini ya mwanzo** ili uchague programu unayoiepnda zaidi.

**Kufunga au kufungua mpangilio wako wa skrini ya mwanzo:**

Baada ya mpangilio wa skrini ya mwanzo kufungwa, huwezi kuongeza/kuondoa/kusawazisha paneli ya skrini ya mwanzo au kuongeza/kuondoa/kuhamisha vipengele vilivyo kwenye skrini ya mwanzo.

1. Gusa na ushikilie sehemu tupu ya skrini ya mwanzo ili ufikie vijipicha vya skrini ya mwanzo.
2. Gusa / ili ufunge/ufungue mpangilio wa skrini ya mwanzo.

# Kujua mambo msingi

## Kufuatilia hali ya simu

Mwambaa wa hali ulio juu mwa skrini ya mwanzo unatoa ikoni za hali ya simu na huduma upande wa kulia. Hapa chini kuna baadhi ya ikoni unazoweza kuona.

| | | | |
|---|---|---|---|
| E | EDGE imeunganishwa |  | Hakuna wimbi |
| 3G / H+ | 3G/HSPA+ imeunganishwa |  | Nguvu ya wimbi |
| 4G | 4G imeunganishwa |  | Modi ya ndege |
|  | Modi ya usinisumbue imewashwa (Ving'ora peke yake au Vipaumbele peke yake) |  | Bluetooth® imewashwa |
|  | Modi ya usinisumbue imewashwa (Kimya kabisa) |  | Imeunganishwa kwenye mtandao wa Wi-Fi® |
|  | Mtetemo umewashwa |  | Spika imewashwa |
|  | Nishati ya betri iko chini |  | Mikrofoni ya simu imezimwa |
|  | Betri limejaa |  | GPS imewashwa |
|  | Betri linachaji |  | King'ora kimewekwa |
|  | Kihifadhi data kimewashwa |  | Wi-Fi ya kubebeka imewashwa |
|  | Kipokea sauti cha waya kimeunganishwa | | |

# Kudhibiti taarifa

## Ikoni za taarifa

Mwambaa wa hali ulio juu mwa skrini ya mwanzo unaonyesha ikoni za taarifa upande wa kushoto. Hapa chini kuna baadhi ya ikoni unazoweza kuona.

| | | | |
|---|---|---|---|
| | SMS/MMS mpya | | Mtandao mpya wa Wi-Fi umegunduliwa |
| / | Ujumbe mpya kutoka programu ya Gmail™ | | Kupakua data |
| / | Ujumbe mpya kutoka programu ya Email | | Kutuma data |
| | Simu uliyokosa kushika | | Muunganisho wa USB umewashwa |
| | Simu inaendelea | | Kadi ya microSD imeunganishwa |
| | Simu inasubiri | | Wimbo unaocheza |

## Fungua/funga paneli ya taarifa

Taarifa zinaripoti kuwasili kwa ujumbe mpya, matukio ya kalenda, na ving'ora, pamoja na matukio yanayoendelea, kama vile unapocheza muziki. Unaweza kufungua paneli ya taarifa ili utazame maelezo ya taarifa.

- Ili ufungue paneli ya taarifa, telezesha kidole chako chini kutoka juu mwa skrini.
- Kufunga paneli ya taarifa, telezesha kidole chako juu kwenye skrini au gusa .

# Kuingiza maandishi

Unaweza kuingiza maandishi kwa kutumia kibodi ya skrini. Baadhi ya programu huifungua kiotomatiki. Katika programu zingine unaifungua kwa kugusa sehemu unayotaka kucharaza. Gusa ▼ ufiche kibodi ya skrini. Unaweza pia kuingiza maandishi kwa kuzungumza na kipengele cha kucharaza sauti cha Google.

## Wezesha au lemaza mbinu za ingizo

1. Gusa ◉ > ⋯ > **Mipangilio > Lugha na ingizo > Kibodi mnemba**.
2. Gusa **Dhibiti kibodi**.
3. Telezesha swichi zilizo kando ya mbinu za ingizo ili uziwezeshe au uzilemaze.

**DOKEZO:**

Baadhi ya mbinu chaguo-msingi za ingizo huenda zisilemazwe.

## Badilisha mbinu za ingizo

1. Wakati unatumia kibodi ya skrini kuingiza maandishi, gusa ikoni ⌨ iliyo kwenye kona ya upande wa chini kulia mwa skrini.
2. Chagua mbinu ya ingizo unayohitaji.

**DOKEZO:**

Ikoni ⌨ hiyo inaonekana tu wakati zaidi ya mbinu moja ya ingizo zimesakinishwa na kuwezeshwa.

## Mipangilio ya mbinu ya ingizo

Chagua mipangilio ya mbinu ya ingizo kwa kugusa ⋯ > **Mipangilio > Lugha na ingizo > Kibodi mnemba** kutoka kwenye skrini ya mwanzo. Unaweza kuweka mbinu ya sasa ya ingizo na uchague mipangilio ya mbinu za ingizo.

# Kuhariri maandishi

- **Sogeza kidosa cha uingizaji:** Gusa sehemu unayotaka kucharaza. Kidosa kinapepesa katika nafasi mpya, na kichupo kinaonekana chini yake. Kokota kichupo ili usogeze kidosa.

- **Chagua maandishi:** Gusa na ushikilie au uguse mara mbili ndani ya maandishi. Neno lililokaribu kabisa linaangaziwa, na kichupo katika kila mwisho wa uteuzi. Kokota vichupo ili ubadilishe uteuzi.
- **Kata au nakili:** Chagua maandishi unayotaka kunakili.. Kisha gusa **KATA** au **NAKILI** ili ukate au unakili maandishi kwenye ubao pogoa.
- **Badilisha maandishi na maandishi yaliyo kwenye ubao pogoa:** Chagua maandishi unayotaka kubadilisha. Kisha gusa **CHAPISHA**.
- **Ingiza maandishi yaliyo kwenye ubao pogoa kwenye kipengele cha maandishi:** Gusa na ushikilie kichupo kilicho chini mwa kidosa na kisha uchague **CHAPISHA**.

# Kufungua na kubadilisha programu

## Fungua programu

1. Gusa > ili ufungue skrini ya orodha ya programu.
2. Telezesha juu au chini kwenye skrini na uguse programu ili uifungue.

**DOKEZO:**

Kokota slaida iliyo upande wa kulia wa skrini kwenye herufi ya kwanza ya programu unayohitaji, au gusa kisanduku cha utafutaji kilicho juu upande wa juu ili utafute programu.

## Badilisha kati ya programu zilizofunguliwa hivi karibuni

1. Gusa . Programu ulizotumia hivi karibuni zinaonyeshwa katika mfululizo wa vichupo. Telezesha juu na chini ili uone vichupo vyote.
2. Gusa kichupo ili ufungue programu hiyo.

**DOKEZO:**

Unaweza kutelezesha kichupo kandokando au uguse **X** iliyo kwenye kichupo ili ukiondoe kutoka kwenye skrini; gusa iliyo kwenye kichupo ukifunge; gusa **FUTA ZOTE** ili uondoe vichupo vyote ambavyo havijafungwa.

**DOKEZO:**

Gusa mara mbili ili ubadilishe kati ya programu mbili zilizofunguliwa hivi karibuni kabisa haraka.

## Tumia programu mbili katika modi ya skrini iliyogawanywa

Unaweza kutumia programu mbili kwa wakati mmoja katika modi ya skrini iliyogawanywa.

**DOKEZO:**

Baadhi ya programu huenda zisikubali modi ya skrini iliyogawanywa.

1. Fungua programu ya kwanza unayotaka kutumia na kisha uguse na ushikilie . Skrini imegawanywa mara mbili.
2. Unaweza kufanya moja ya mambo yanayofuata.
   - Ikiwa programu unayohitaji iko katika orodha ya programu za hivi karibuni, iguse ili uiweke kama programu ya pili.
   - Gusa > ili upate programu unayohitaji na uifungue kama programu ya pili.

Kuzima modi ya skrini iliyogawanywa, gusa na ushikilie , au kokota kishikio kilicho kwenye skrini hadi ukingo wa skrini.

## Kusakinusha programu

1. Gusa > ufungue skrini ya orodha ya programu.
2. Gusa na ushikilie ikoni ya programu na ukokote ikoni hiyo kwenye **(Sakinusha)** juu mwa skrini.
3. Gusa **SAWA** ili usakinushe programu.

**DOKEZO:**

Programu zilizosakinishwa kabla haziwezi kusakinushwa.

## Kuficha programu

Unaweza kuficha programu katika skrini ya orodha ya programu.

1. Gusa > ili ufungue skrini ya orodha ya programu.
2. Gusa **> Ficha programu**.
3. Gusa programu unayotaka kuficha na uguse .

**DOKEZO:**

Gusa > > **> Ficha programu** ili utazame programu zote zilizofichwa hapa juu. Unaweza kugusa programu zilizofichwa na uguse ili uzionyeshe tena katika skrini ya orodha ya programu.

# Kuunganisha kwenye mitandao na vifaa

## Kuunganisha kwenye mitandao rununu

### Dhibiti matumizi ya SIM mbili

Gusa > > **Mipangilio > kadi za SIM**. Unaweza kudhibiti majina ya kadi ndogo za SIM, kuwezesha au kulemaza kadi au data, au kuweka unayopendelea kutumia kwa data, simu, au ujumbe.

- Gusa jina la kadi ndogo ya SIM (kadi chaguo-msingi ni SIM 1 na SIM 2) ili ubadilishe jina au rangi, au uangalie mtoa huduma na nambari.
- Gusa swichi iliyo kando ya majina ya kadi uwezeshe au ulemaze kadi.
- Gusa **Data rununu** ili uwezeshe au ulemaze data rununu ya kadi zote mbili.
- Gusa **Data ya simu, Simu,** au **Ujumbe wa SMS** uchague kadi unayopendelea kutumia kwa kila shughuli.

### Dhibiti matumizi ya data rununu

**Kuwezesha au kulemaza ufikiaji wa data:**

1. Gusa > > **Mipangilio > Matumizi ya data**.
2. Gusa swichi ya **Data rununu** iliyo chini mwa **SIM 1 ya Rununu** au **SIM 2 ya Rununu** ili uwezeshe au ulemaze matumizi ya data rununu kwa kila kadi ndogo ya SIM.

**Kupata huduma za data wakati unatambizi:**

1. Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > Mitandao rununu**.
2. Ikiwa kadi mbili ndogo za SIM zimeingizwa, gusa kichupo cha kadi moja.
3. Gusa swichi ya **Utambizi wa data** ikiwa imezimwa.

**DOKEZO:**

Utambizi wa data unaweza kusababisha gharama kubwa ya utambizi.

## Chagua aina ya mtandao unayoipendelea

1. Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > Mitandao rununu**.
2. Ikiwa kadi mbili ndogo za SIM zimeingizwa, gusa kichupo cha kadi moja.
3. Gusa **Aina ya mtandao unayoipendelea** na uguse aina ya mtandao unayopendelea simu kuunganishwa.

## Weka majina ya vituo vya ufikiaji

Kuunganisha kwenye Wavuti unaweza kutumia Majina Chaguo-msingi ya Vituo vya Ufikiaji (APN). Na ikiwa unataka kuongeza APN mpya, tafadhali wasiliana na mtoa huduma upate taarifa muhimu.

1. Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > Mitandao rununu**.
2. Ikiwa kadi mbili ndogo za SIM zimeingizwa, gusa kichupo cha kadi moja.
3. Gusa **Majina ya vituo vya ufikiaji** na kisha uguse .
4. Gusa kila kipengele ili uingize taarifa unayopata kutoka kwa mtoa huduma wako.
5. Gusa > **Hifadhi** ili ukamilishe.

**DOKEZO:**

Kuweka APN kwa mipangilio chaguo-msingi, gusa > **Weka upya kwa chaguo-msingi**.

## Chagua mtoa huduma wa mtandao

1. Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > Mitandao rununu**.
2. Ikiwa kadi mbili ndogo za SIM zimeingizwa, gusa kichupo cha kadi moja.
3. Gusa **Watoa huduma wa mtandao**.
4. Gusa **Tafuta mitandao** ili utafute mitandao yote inayopatikana.
5. Gusa mtandao katika orodha ya mitandao ili usajili mwenyewe.

   Unaweza pia kugusa **Chagua kiotomatiki** ili uchague mtandao unaoupendelea kiotomatiki.

# Kuunganisha kwenye Wi-Fi

Wi-Fi ni teknolojia pasi waya ya mtandao inayoweza kutoa ufikiaji wa Wavuti wa hadi mita 100, kulingana na ruta ya Wi-Fi na mazingira yako.

## Washa Wi-Fi na uunganishe kwenye mtandao wa Wi-Fi

1. Gusa > > **Mipangilio > Wi-Fi**.
2. Telezesha swichi ya **Wi-Fi** kwenye nafasi ya **Washa** ili uwashe Wi-Fi.
3. Gusa jina la mtandao ili uunganishe kwenye mtandao huo.
4. Ikiwa mtandao ni salama, ingiza nenosiri na uguse **UNGANISHA**.

**DOKEZO:**

Simu yako inaunganisha kiotomatiki kwenye mitandao ya Wi-Fi uliyotumia hapo awali ikiwa iko karibu.

## Pata arifa kuhusu mitandao wazi

1. Gusa > > **Mipangilio > Wi-Fi**.
2. Telezesha swichi ya **Wi-Fi** kwenye nafasi ya **Washa**.
3. Gusa .
4. Telezesha swichi ya **Taarifa ya mtandao**.

Wakati Wi-Fi imewashwa, utapokea taarifa katika mwambaa wa hali wakati simu yako inagundua mtandao wazi wa Wi-Fi. Zima chaguo hili ili uzime taarifa.

## Ongeza mtandao wa Wi-Fi

Unaweza kuongeza mtandao wa Wi-Fi ikiwa mtandao huo hautangazi jina lake (SSID), au kuongeza mtandao wa Wi-Fi wakait uko mbali.

Kuunganisha kwenye mtandao salama, kwanza unahitaji kupata maelezo ya usalama kutoka kwa msimamizi wa mtandao.

1. Gusa > > **Mipangilio > Wi-Fi**.
2. Telezesha swichi ya **Wi-Fi** kwenye nafasi ya **Washa**.
3. Gusa **Ongeza mtandao** chini mwa orodha ya mitandao ya Wi-Fi.

4. Ingiza SSID ya mtandao (jina). Ikihitajika, ingiza maelezo ya usalama na usanidi mwingine wa mtandao.
5. Gusa **HIFADHI**.

## Unganisha kwenye mtandao wa WPS

Usanidi wa Wi-Fi Uliolindwa (WPS) ni kipengele kinachorahisisha kuongeza simu yako kwenye vituo vya ufikiaji vinavyokubali WPS.

Unaweza kutumia moja ya mbinu zinazofuata kuunganisha simu yako kwenye mtandao pasi waya ukitumia WPS.

**Mbinu ya kwanza: Kitufe cha WPS (Inapendekezwa)**

1. Gusa **> > Mipangilio > Wi-Fi**.
2. Telezesha swichi ya **Wi-Fi** kwenye nafasi ya **Washa**.
3. Gusa **> Mahiri > Kitufe cha Uwasilishaji cha WPS**.
4. Bonyeza kitufe cha WPS kilicho kwenye kituo cha ufikiaji na kituo cha ufikiaji kitatambua simu yako na kuiongeza kwenye mtandao.

**Mbinu ya pili: Nambari ya PIN**

1. Gusa **> > Mipangilio > Wi-Fi**.
2. Telezesha swichi ya **Wi-Fi** kwenye nafasi ya **Washa**.
3. Gusa **> Mahiri > Uingizaji wa PIN ya WPS**.
4. Nambari ya PIN ya WPS huonyeshwa kwenye skrini. Ingiza nambari ya PIN kwenye ukurasa wa usanidi wa kituo cha ufikiaji.

Baada ya kuingiza nambari ya PIN, simu yako itatafuta kituo cha ufikiaji kiotomatiki na kusanidi muunganisho.

**DOKEZO:**

Kwa maelezo kamili kuhusu kipengele cha WPS cha kituo cha ufikiaji, tafadhali pitia hati zake za watumiaji.

## Sahau mtandao wa Wi-Fi

Unaweza kufanya simu yako isahau kuhusu maelezo ya mtandao wa Wi-Fi uliouongeza - kwa mfano, ikiwa hutaki simu kuunganishwa kwake kiotomatiki au ikiwa ni mtandao ambao huwa huutumii.

1. Gusa **> > Mipangilio > Wi-Fi**.
2. Telezesha swichi ya **Wi-Fi** kwenye nafasi ya **Washa**.

3. Gusa ⚙ na uguse **Mitandao iliyohifadhiwa**.
4. Gusa jina la mtandao wa Wi-Fi na kisha uguse **SAHAU**.

## Unganisha kwenye kifaa kingine kupitia Wi-Fi Direct®

Wi-Fi Direct huruhusu vifaa vya Wi-Fi kushiriki faili na data moja kwa moja kwa kuungana bila mahitaji ya vituo vya ufikiaji vya pasi waya (maeneo ya Wavuti).

1. Gusa ◉ > ⠿ > **Mipangilio > Wi-Fi**.
2. Ikiwa Wi-Fi imezimwa, telezesha swichi ya **Wi-Fi** kwenye nafasi ya **Washa**.
3. Gusa ⋮ > **Mahiri > Wi-Fi Direct**. Simu yako itatafuta vifaa vingine vyenye miunganisho ya Wi-Fi Direct.
4. Gusa jina la kifaa chini ya **Vifaa rika** ili uunganisha kwake.

   Kifaa hicho kinigne kitapokea agizo la muunganisho na kinahitaji kukubali agizo hili la muunganisho. Huenda vifaa vyote viwili vikahitaji uingize PIN sawa.
5. Kikishaunganishwa kifaa kinaonyeshwa kama “Kimeunganishwa” katika orodha ya **Vifaa rika**.

## Kuunganisha vifaa vya Bluetooth

Bluetooth ni teknolojia pasi waya ya mawasiliano ya karibu. Simu au vifaa vingine vyenye uwezo wa Bluetooth vinaweza kubadilishana taarifa bila muunganisho wa waya ndani ya umbali wa takriban mita 10 (fiti 32.8). Lazima vifaa vya Bluetooth viunganishwe kabla ya mawasiliano kufanyika.

### Washa/zima Bluetooth

1. Gusa ◉ > ⠿ > **Mipangilio > Bluetooth**.
2. Telezesha swichi ya **Bluetooth** kwenye nafasi ya **Washa** au **Zima**.

Wakati Bluetooth imewashwa, ikoni ya ✱ inaonekana katika mwambaa wa hali.

## Badilisha jina la kifaa

1. Gusa  >  > **Mipangilio > Bluetooth**.
2. Telezesha swichi ya **Bluetooth** kwenye nafasi ya **Washa** ikiwa Bluetooth imezimwa.
3. Gusa  > **Badilisha jina la kifaa hiki**.
4. Hariri jina na uguse **BADILISHA JINA**.

## Oanisha na kifaa kingine cha Bluetooth

1. Gusa  >  > **Mipangilio > Bluetooth**.
2. Telezesha swichi ya **Bluetooth** kwenye nafasi ya **Washa** ikiwa Bluetooth imezimwa.

   Siku yako hutafuta na kuonyesha vitambulisho vya vifaa vyote vya Bluetooth vilivyokaribu kiotomatiki. Unaweza kugusa  > **Pakia upya** ikiwa unataka kutafuta tena.
3. Gusa kifaa unachotaka kuoanisha nacho.
4. Thibitisha kwamba manenosiri ya Bluetooth yanalingana kati ya vifaa hivyo viwili na uguse **OANISHA**. Vinginevyo, ingiza nenosiri la Bluetooth na uguse **OANISHA**.

   Uonanishaji umefauli wakati kifaa hicho kingine kinakubali muunganisho huo au wakati nenosiri sawa limeingizwa.

**DOKEZO:**

Nenosiri la Bluetooth huenda likawa la kudumu kwa vifaa fulani kama vile vipokea suati na vifaa visivyo vya kushikilia kwa mkono vya gari. Unaweza kujaribu kuingiza 0000 au 1234 (manenosiri yanayotumika mara nyingi zaidi), au upitie hati za kifaa hicho.

## Sahau (tenganisha kutoka kwa) kifaa cha Bluetooth

Unaweza kufanya simu kusahau muunganisho wako wa uoanishaji na kifaa kingine cha Bluetooth. Kuunganisha kwenye kifaa hicho tena, unahitaji kukitafuta na kuingiza au kuthibiitsha nenosiri tena.

1. Gusa  >  > **Mipangilio > Bluetooth** na uhakikishe kwamba Bluetooth imewashwa.
2. Katika orodha ya vifaa vilivyooanishwa, gusa ikoni  iliyo kando mwa kifaa cha Bluetooth unachotaka kusahau.
3. Gusa **SAHAU**.

### Tuma data kupitia Bluetooth

1. Fungua programu inayofaa na uchague faili au kipengele unachotaka kushiriki.
2. Chagua chaguo la kushiriki kupitia Bluetooth. Mbinu hizo huenda zikatofautiana na programu na aina ya data.
3. Gusa kifaa cha Bluetooth ambacho simu imeoanishwa nacho au uisubiri itafute vifaa vipya na uguse kimoja.

### Pokea data kupitia Bluetooth

1. Washa Bluetooth kabla ya kujaribu kupokea data kupitia Bluetooth.
2. Gusa **KUBALI** ili uanze kupokea data. Ikihitajika, vuta mwambaa wa hali chini, gusa **KUBALI** kwenye taarifa ya kushiriki Bluetooth.

Faili zinazopokewa zinahifadhiwa kiotomatiki katika folda iliyoteuliwa (**bluetooth**, kwa mfano) katika simu. Unaweza kuzifikia na programu ya **Kidhibiti Faili**.

## Kuunganisha kwenye kompyuta yako kupitia USB

Unaweza kuunganisha simu yako kwenye kompyuta ukitumia kebo ya USB na kuhamisha muziki, picha, na faili zingine pande zote mbili. Simu yako huzihifadhi faili hizi katika hifadhi ya ndani au kwenye kadi ya microSD inayoweza kutolewa.

Ikiwa unatumia muunganisho wa USB, lazima uuzime kabla ya uweze kutumia uhamishaji wa faili wa USB kati ya simu na kompyuta yako.

### Unganisha simu yako kwenye kompyuta kupitia USB

1. Unganisha simu yako kwenye kompyuta ukitumia kebo ya USB.
2. Fungua paneli ya taarifa na uguse **(USB...)**.
3. Chagua moja ya chaguo zinazofuata:
   - **Kuchaji kifaa hiki:** Chaji simu yako kupitia USB.
   - **Hamisha faili:** Hamisha faili kwenye Windows® au Mac®.

**DOKEZO:**

Kwa Windows XP, tafadhali sakinisha Media Player 11 (au toleo la baadaye) unapotumia MTP.

- **Hamisha picha (PTP):** Hamisha picha au faili ikiwa MTP haikubaliwi na kompyuta yako.

### Tenganisha simu yako kutoka kwenye kompyuta

Kutenganisha simu kutoka kwenye kompyuta, chomoa kebo ya USB unapomaliza.

## Kutumia kadi ya microSD kama hifadhi ya kubebeka au ya ndani

Unaweza kutumia kadi ya microSD kama hifadhi ya kubebeka wakati tayari kuna maudhui kama vile media yako na faili zingine ili usizipoteze.

Ikiwa kadi yako ya microSD ni mpya au haina maudhui unayotaka kuyahifadhi, unaweza pia kuiweka kama nyongeza ya hifadhi ya ndani, jambo ambalo linahitaji uwekaji utakaouzuia kadi ya microSD kufanya kazi na vifaa vingine.

**TAHADHARI:**

Kama sehemu ya hifadhi ya ndani, kadi ya microSD inaweza kuwa na data ndani yake inayohitajika na baadhi ya programu ili zifanye kazi vizuri. Kwa hivyo, usiondoe au kubadilisha kadi kiholela.

### Weka kadi ya microSD kama hifadhi ya kubebeka

Unaposakinisha kadi ya microSD ambayo haijawahi kutumiwa kwenye kompyuta yako, simu itaunganisha kadi hiyo kama hifadhi ya kubebeka kwa chaguo-msingi.

Pia unaweza kufungua paneli ya taarifa na uguse jina la kadi ya microSD, uchague **Tumia kama hifadhi ya kubebeka** na kisha uguse **INAYOFUATA > MALIZA**.

#### Kuondoa kadi ya microSD kutoka kwenye simu yako:

Ikiwa unahitaji kuondoa kadi ya microSD inayotumika kama hifadhi ya kubebeka simu ikiwa imewashwa, lazima uitenganishe kwanza.

1. Gusa > > **Mipangilio > Bluetooth**.

2. Gusa ⏏ iliyo kando ya jina la kadi katika fungu la **Hifadhi ya kubebeka**.
3. Wakati skrini inaonyesha kwamba kadi imechomolewa kwa usalama, sasa unaweza kuiondoa kutoka kwenye simu.

**Kufuta na kufomati kadi ya microSD:**

1. Gusa ● > ⋯ > **Mipangilio** > **Hifadhi**.
2. Gusa jina la kadi katika fungu la **Hifadhi ya kubebeka**.
3. Gusa ⋮ > **Mipangilio ya hifadhi** na kisha uguse **Fomati**.
4. Gusa **FUTA NA FOMATI**.

**TAHADHARI:**

Utaratibu ya kufomati hufuta data yote iliyo kwenye kadi ya microSD, na kisha faili hizo HAZITAWEZA kuepuliwa.

## Weka kadi ya microSD kama hifadhi ya ndani

Ikiwa kadi yako ya microSD ni mpya au haina maudhui unayotaka kuhifadhi, unaweza kufomati kadi hiyo na kuitumia kama sehemu ya hifadhi ya ndani. Ukihamisha kadi ya microSD kwenye kifaa kingine, itafomatiwa kabla ya kutumiwa.

1. Gusa ● > ⋯ > **Mipangilio** > **Hifadhi**.
2. Gusa jina la kadi katika fungu la **Hifadhi ya kubebeka**.
3. Gusa ⋮ > **Mipangilio ya hifadhi** na kisha uguse **Fomati kama ya ndani**.
4. Gusa **FUTA NA FOMATI**.

   **TAHADHARI:**

   Utaratibu ya kufomati hufuta data yote iliyo kwenye kadi ya microSD, na kisha faili hizo HAZITAWEZA kuepuliwa.
5. Simu itakuambia uhamishe picha, faili na data yako nyingine kutoka hifadhi ya ndani kwenye kadi ya microSD. Chagua **Hamisha** na ufuate maelekezo yaliyo kwenye skrini, au gusa ◀ ili uhamishe baadaye.

**Kuhamisha data kati ya hifadhi ya ndani na kadi ya microSD:**

Ukiwa na kadi ya microSD kama sehemu ya hifadhi ya ndani, unaweza kuhamisha picha, faili na data yako nyingine kati ya hifadhi ya ndani na kadi hiyo wakati wowote.

1. Gusa ● > ⋯ > **Mipangilio** > **Hifadhi**.

2. Gusa **Hifadhi ya ndani inayoshirikishwa** au jina la kadi ya microSD.
3. Gusa ⋮ > **Hamisha data**.
4. Gusa **HAMISHA**.

**DOKEZO:**

Wakati wowote unaohamisha data kati ya hifadhi ya ndani na kadi ya microSD, hifadhi unayohamishia data inatumiwa kuhifadhi programu mpya na data ya kibinafsi (kama vile picha na video) na ni hifadhi hiyo unayohamishia data tu inaweza kufikiwa kutoka kwenye kompyuta.

**Kuondoa kadi ya microSD kutoka kwenye simu yako:**

Ikiwa unahitaji kuondoa kadi ya microSD inayotumika kama hifadhi ya ndani simu ikiwa imewashwa, lazima uitenganishe kwanza.

1. Gusa > > **Mipangilio > Hifadhi**.
2. Gusa jina la kadi yako chini ya **Hifadhi ya ndani inayoshirikishwa**.
3. Gusa ⋮ > **Chomoa**.

   **DOKEZO:**

   Kabla ya kuchomoa kadi, hakikisha kwamba umehamisha data na programu kwenye hifadhi ya ndani.
4. Gusa **CHOMOA**.
5. Wakati skrini inaonyesha kwamba kadi imechomolewa kwa usalama, sasa unaweza kuiondoa kutoka kwenye simu.

**Kufomati kadi ya microSD upya kama hifadhi ya kubebeka:**

Ikiwa hutaki kutumia kadi yako ya microSD kama hifadhi ya ndani tena, unaweza kuifomati kadi hiyo kama hifadhi ya kubebeka.

**DOKEZO:**

Kabla ya kufomati, hakikisha kwamba umehamisha data na programu kwenye hifadhi ya ndani.

1. Gusa > > **Mipangilio > Hifadhi**.
2. Gusa jina la kadi yako chini ya **Hifadhi ya ndani inayoshirikishwa**.
3. Gusa ⋮ > **Fomati kama ya kubebeka**.

4. Gusa **FOMATI**.

**TAHADHARI:**

Utaratibu ya kufomati hufuta data yote iliyo kwenye kadi ya microSD, na kisha faili hizo HAZITAWEZA kuepuliwa.

# Kushiriki muunganisho wako wa data rununu

Unaweza kushiriki data ya simu yako kupitia muunganisho au kwa kuamilisha kipengele cha Wi-Fi ili uunde wavuti rununu.

## Shiriki muunganisho wako wa data rununu kupitia USB

Unaweza kufikia Wavuti kwenye kompyuta yako kupitia kipengele cha muunganisho wa USB cha simu yako. Kipengele hiki kinahitaji muunganisho wa data kwenye mtandao rununu na kunaweza kusababisha gharama ya data.

**DOKEZO:**

Huwezi kuhamisha faili kati ya simu yako na kompyuta yako wakati simu imeunganishwa kupitia USB.

1. Unganisha simu yako kwenye kompyuta ukitumia kebo ya USB.
2. Gusa > **> Mipangilio > Zaidi > Eneo wavuti la kuunganisha na kubebeka**.
3. Washa **Muunganisho wa USB**. Muunganisho mpya wa mtandao utaundwa kwenye kompyuta yako.

**DOKEZO:**

Kuwacha kushiriki muunganisho wako wa data, zima **Muunganisho wa USB** au tenganisha kebo ya USB.

## Shiriki muunganisho wako wa data rununu kupitia Bluetooth

Ikiwa kompyuta yako inaweza kupata muunganisho wa Wavuti kupitia Bluetooth, unaweza kusanidi simu yako kushiriki muunganisho wake wa data rununu na kompyuta yako.

1. Oanisha simu yako na kompyuta yako kupitia Bluetooth.
2. Sanidi kompyuta yako ili upate muunganisho wake wa mtandao kupitia Bluetooth. Kwa maelezo zaidi, tafadhali angalia hati za kompyuta yako.

3. Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > Eneo wavuti la kuunganisha na kubebeka**.
4. Washa **Muunganisho wa Bluetooth.** Sasa kompyuta yako inashiriki muunganisho wa data wa simu yako.

**DOKEZO:**

Kuwacha kushiriki muunganisho wako wa data, zima **Muunganisho wa Bluetooth**.

## Shiriki muunganisho wako wa data rununu kama Wi-Fi

Unaweza kushiriki muunganisho wa data wa simu yako na vifaa vingine kwa kufanya simu yako kuwa Wi-Fi ya kubebeka. Kipengele hiki kinahitaji muunganisho wa data kwenye mtandao rununu na kunaweza kusababisha gharama ya data.

**DOKEZO:**

Wakati kipengele cha Wi-Fi ya kubebeka kimewezeshwa, huwezi kutumia uwezo wa Wi-Fi wa simu yako kufikia Wavuti. Bado utaendelea kuunganishwa kwenye Wavuti kupitia mtandao wako wa data rununu.

1. Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > Eneo wavuti la kuunganisha na kubebeka**.
2. Washa **Wi-Fi ya kubebeka**.

   Baada ya muda mfupi, simu yako itaanza kutangaza jina la mtandao wake wa Wi-Fi (SSID).
3. Kwenye kifaa kingine, tafuta simu yako kupitia Wi-Fi na uunganisha nayo ili uanze kutumia data rununu ya simu.

**DOKEZO:**

Kuwacha kushiriki muunganisho wako wa data, zima **Wi-Fi ya kubebeka.**

## Weka Wi-Fi yako

Unaweza kubadilisha jina la mtandao wa Wi-Fi wa simu yako (SSID), kulinda Wi-Fi yako ya kubebeka, na kuweka chaguo zingine.

1. Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > Wi-Fi ya kuunganisha na kubebeka**.
2. Gusa **Weka Wi-Fi** na uweke jina lako na chaguo za usalama

ifuatavyo.

- **Jina la mtandao:** Ingiza au hariri SSID ya mtandao (jina) ambayo vifaa vingine vitaona wakati vinatafuta mitandao ya Wi-Fi.
- **Usalama:** Teua chaguo la usalama. **Hamna** (haipendekezwe) au **WPA2 PSK** (watumiaji wengine wanaweza kufikia Wi-Fi yako tu ikiwa wataingiza nenosiri sahihi). Ukichagua **WPA2 PSK**, gusa kipengele cha **Nenosiri** ili uhariri nenosiri la usalama.

3. Gusa **HIFADHI** ili uhifadhi mipangilio yako.

**DOKEZO:**

Katika skrini ya **Wi-Fi ya kuunganisha na kubebeka**, unaweza pia kuweka sera ya kulala ya Wi-Fi.

## Kuunganisha kwenye mitandao mnemba ya kibinafsi

Mitandao mnemba ya kibinafsi (VPN) hukuruhusu kuunganisha kwenye rasilimali ndani ya mtandao salama wa ndani. VPN hutumiwa sana na mashirika, shule, na taasisi zingine kuwawezesha watu kufikia rasilimali za mtandao wa ndani wakati hawako katika jengo au wakiwa wameunganishwa kwenye mtandao pasi waya.

Kulingana na aina ya VPN unayotumia, unaweza kuhitajika kuingiza maelezo yako ya kuingia au kusakinisha vyeti vya usalama kabla ya kuweza kuunganisha kwenye VPN yako. Unaweza kupata maelezo haya kutoka kwa msimamizi wako wa mtandao.

### Ongeza VPN

1. Gusa ⚪ > ⋯ > **Mipangilio > Zaidi > VPN**.
2. Gusa + iliyo kwenye kona ya juu kulia na ujaze maelezo yaliyotolewa na msimamizi wako wa mtandao.
3. Gusa **HIFADHI**.

VPN imeongezwa kwenye orodha iliyo kwenye skrini ya VPN.

**DOKEZO:**

Lazima uweke mchoro, PIN au nenosiri la kufunga skirni kabla ya kutumia VPN.

## Unganisha kwenye VPN

1. Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > VPN**.
2. Gusa VPN unayotaka kuunganisha nayo.
3. Ukiagizwa, andika maelezo yoyote yaliyoagizwa, na kisha uguse **UNGANISHA**.

## Rekebisha VPN

1. Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > VPN**.
2. Gusa iliyo kando ya VPN unayotaka kurekebisha.
3. Hariri mipangilio ya VPN na kisha uguse **HIFADHI**.

# Simu

Unaweza kupiga simu kutoka kwenye Programu ya Simu, Proramu ya Anwani, au programu na wiji zingine zinazoonyesha maelezo ya anwani. Wakati wowote unaona nambari ya simu, unaweza kuigusa ili kudayo.

## Kupiga na kukata simu

### Piga simu kwa kudayo

1. Gusa > .
2. Gusa na uingize nambari ya simu au jina la anwani ukitumia padi ya kudayo. Gusa ili ufute tarakimu zisizo sahihi.

   **DOKEZO:**

   Unapoingiza nambari ya simu au jina la anwani, simu yako itatafuta maelezo yanayolingana katika anwani zako. Ukiona nambari na anwani unayotaka kupigia simu, iguse ili upige simu mara moja.
3. Gusa iliyo chini mwa kipadi ili udayo.

**DOKEZO:**

Kupiga simu ya kimataifa gusa na ushikilie kibonye cha 0 ili uingize alama ya jumlisha (+). Kisha, ingiza msimbo wa nchi, ukifuatwa na msimbo wa mji/eneo na kisha nambari ya simu.

**DOKEZO:**

Kudayo tena simu uliyopiga mara ya mwisho, gusa > > > na uguse tena.

### Kata simu

Wakati simu inaendelea, gusa kwenye skrini.

## Kujibu au kukataa simu

Unapopokea simu, skrini ya simu inayoingia inafunguka, ikionyesha utambulisho wa mpigaji simu au maelezo kuhusu mpigaji simu uliyohifadhi katika Programu ya Anwani. Unaweza kujibu au kakataa simu, au kuikataa na ujumbe mfupi.

## Jibu simu

Unapopokea simu, kokota juu mwa ili ujibu simu.

\- au -

Ikiwa skrini imefunguliwa, gusa **JIBU** ili ujibu simu.

**DOKEZO:**

Kunyazisha mlio kabla ya kujibu simu bonyeza upande wowote wa mwisho wa kibonye cha **Kiwango-sauti**.

## Kataa simu

Unapopigiwa simu, kokota juu mwa ili uikatae simu.

Pia unaweza kukokota juu mwa ili ukatae simu na uchague ujumbe mfupi uliowekwa awali au uhariri ujumbe mmoja umtumie mpigaji simu.

\- au -

Ikiwa skrini imefunguliwa, gusa **PUUZA** ili ukatae simu.

**DOKEZO:**

Kuhariri jibu la ujumbe uliowekwa awali ndani mwa Programu ya Simu, gusa na uchague **Mipangilio > Majibu ya haraka**.

# Kutumia historia ya simu

Historia ya simu ni orodha ya simu zote ulizopiga, ulizopokea, au ulizokosa. Inatoa njia rahisi ya kudayo nambari upya, kurudisha simu, au kuongeza nambari kwenye anwani zako.

Ili ufungue historia ya simu, unaweza kugusa **>** **>** (katika kipengele cha utafutaji cha upande wa juu) **> Historia ya simu.**

## Piga simu kutoka kwenye historia ya simu

1. Fungua historia ya simu.
2. Gusa iliyo kando ya anwani unayotaka kupigia simu.

### Chukua hatua zingine kwenye ingizo la historia ya simu

Fungua historia ya simu, unaweza kuchukua mambo yanayofuata.

- Gusa ikoni ya anwani mbele mwa orodha uongeze nambari hiyo kwenye anwani au ukague maelezo ya anwani.
- Gusa anwani ili uunde anwani mpya na nambari hiyo, uongeze nambari kwenye anwani iliyopo, utume ujumbe, au upitie maelezo ya simu.
- Gusa na ushikilie anwani ili unakili nambari, uhariri nambari kabla ya kuipigia simu, au uzuie nambari kuwasiliana na wewe.

**DOKEZO:**

Gusa ⋮ > **Futa historia ya simu** katika Historia ya Simu ili ufute rekodi zote za historia.

## Kupigia anwani zako simu

1. Gusa ◉ > 📞.
2. Gusa kichupo cha 👥 ili utazame anwani zako zote, au gusa kichupo cha ★ ili ufikie anwani unazozipenda zaidi au unazowasiliana nazo mara kwa mara.
3. Gusa anwani ili upige simu.

# Anwani

Unaweza kuongeza anwani kwenye simu yako na uzilandanishe na anwani zilizo katika akaunti yako ya Google au akaunti zingine zinazokubali mlandanisho wa anwani.

Kuona anwani zako, gusa > > **Anwani**. Kutoka hapo, unaweza kugusa vichupo vilivyo juu mwa skrini ili uende kwenye anwani unazozipenda zaidi kwa haraka.

## Kuangalia maelezo ya anwani

1. Gusa > > **Anwani** na uguse kichupo cha **ZOTE** ili ufikie orodha yako ya anwani.
2. Biringiza orodha ili utazame anwani zako zote.
3. Gusa anwani ili utazame maelezo yake.

**DOKEZO:**

Ikiwa umehifadhi anwani nyingi, utaona slaida upande wa kulia wa skrini. Kokota slaida hiyo hadi kwenye herufi ya kwanza unayohitaji.

## Kuongeza anwani mpya

1. Gusa > > **Anwani**.
2. Gusa ili uongeze anwani mpya.
3. Gusa **Hifadhi kwenye** ili uchague unapotaka kuhifadhi anwani hiyo. Ikiwa utachagua landanisha akaunti, anwani zitalandanishwa kiotomatiki na akaunti yako mtandaoni.
4. Ingiza jina la anwani, nambari ya simu, anwani ya barua pepe, na maelezo mengine. Gusa **Vipengele zaidi** ikihitajika.
5. Gusa ili uhifadhi anwani.

## Kuunda wasifu wako binafsi

Unaweza kuunda kadi yenye jina lako katika simu yako.

1. Gusa > > **Anwani** na uguse kichupo cha **Zote**.
2. Gusa **Unda wasifu wangu**.

Ikiwa tayari wasifu ushaundwa, gusa kipengele kilicho kando ya **MIMI** na uguse .

3. Hariri maelezo ya wasifu wako.
4. Gusa .

# Kuingiza, kuhamisha, na kushiriki anwani

Unaweza kuingiza/kuhamisha anwani kutoka/kwenye kadi yako ndogo ya SIM, hifadhi ya simu au kadi ya microSD. Hii ni muhimu hasa wakati unahitaji kuhamisha anwani kati ya vifaa tofauti. Pia unaweza kushiriki anwani haraka kwa kutumia Ujumbe, Bluetooth, Gmail, Hifadhi ya Google, nk.

## Ingiza anwani kutoka kwenye kadi ndogo ya SIM

1. Gusa > > **Anwani**.
2. Gusa > **Ingiza/hamisha** > **Ingiza kutoka kwenye kadi ya SIM**.
3. Ikiwa kadi mbili ndogo za SIM zimeingizwa, chagua kadi unayotaka kuingiza anwani kutoka kwake na uguse **SAWA**.
4. Chagua akaunti unayotaka kuhifadhi anwani hizo.
5. Chagua anwani unazohitaji na kisha uguse **Sawa**.
6. Gusa **SAWA** ili uthibitishe.

## Ingiza anwani kutoka hifadhi ya ndani au kadi ya microSD

1. Gusa > > **Anwani**.
2. Gusa > **Ingiza/hamisha** > **Ingiza kutoka faili ya .vcf**.
3. Chagua akaunti unayotaka kuhifadhi anwani hizo.
4. Gusa mahali faili zilizoingizwa za vCard zimehifadhiwa kwenye hifadhi ya simu au kadi ya microSD na uguse moja ili uingize anwani.

## Hamisha anwani kwenye kadi ndogo ya SIM

1. Gusa > > **Anwani**.
2. Gusa > **Ingiza/hamisha** > **Hamisha kwenye kadi ya SIM**.

3. Ikiwa kadi mbili ndogo za SIM zimeingizwa, chagua kadi unayotaka kuhamishia anwani kwake na uguse **SAWA**.
4. Angalia anwani unazohitaji na kisha uguse **Sawa**.

### Hamisha anwani kwenye hifadhi ya ndani au kadi ya microSD

1. Gusa > > **Anwani**.
2. Gusa > **Ingiza/hamisha > Hamisha kwenye faili ya .vcf**.
3. Chagua anwani unazohitaji na kisha uguse **Sawa**.
4. Gusa mahali unapotaka kuhifadhi faili ya vCard.
5. Hariri jina la faili ikiwa inahitajika na uguse **HIFADHI** ili uunde faili.

### Shiriki anwani

1. Gusa > > **Anwani** na uguse kichupo cha **ZOTE**.
2. Gusa na ushikilie anwani unayotaka kushiriki.
3. Chagua anwani zaidi ikiwa inahitajika na kisha uguse > **Shiriki**.
4. Chagua namna ya kushiriki anwani. Chaguo zinategemea programu na huduma zilizosakinishwa.

-au-

1. Gusa > > **Anwani >** > **Ingiza/hamisha > Shiriki anwani zote**.
2. Gusa na ushikilie anwani unayotaka kushiriki.
3. Chagua anwani zaidi ikiwa inahitajika na kisha uguse **Sawa**.
4. Chagua namna ya kushiriki anwani. Chaguo zinategemea programu na huduma zilizosakinishwa.

## Kutumia anwani unazozipenda zaidi

Katika kichupo cha anwani unazozipenda zaidi, unaweza kupata anwani unazozipenda zaidi na anwani za watu unaowasiliana nao zaidi.

### Ongeza anwani kwenye anwani unazozipenda zaidi

Unaweza kuongeza anwani unazotumia mara kwa mara kwenye **UNAZOZIPENDA ZAIDI** ili uweze kuzitafuta haraka.

1. Gusa > > **Anwani** na uguse kichupo cha **Zote**.
2. Gusa anwani na kisha uguse upande wa juu.

### Ondoa anwani kutoka anwani unazozipenda zaidi

1. Gusa > > **Anwani** na uguse kichupo cha **UNAZOZIPENDA ZAIDI**.
2. Gusa anwani unazozipenda zaidi na kisha uguse upande wa juu.

## Kutafuta anwani

1. Gusa > > **Anwani**.
2. Gusa upande wa juu wa skrini.
3. Ingiza jina la anwani au maelezo yoyote ya anwani hiyo ili uitafute. Anwani zinazolingana na maelezo yako ya utafutaji zitaorodheshwa.

## Kuhariri anwani

### Hariri maelezo ya anwani

1. Gusa > > **Awani**.
2. Gusa anwani unayohitaji kuhariri na kisha uguse .
3. Hariri anwani na uguse .

### Futa anwani

1. Gusa > > **Anwani** na uguse kichupo cha **Zote**.
2. Gusa na ushikilie anwani unayotaka kuondoa.
3. Chagua anwani zaidi ikiwa inahitajika na kisha uguse > **Futa**.
4. Gusa **SAWA** ili uthibitishe.

## Unganisha anwani

Kwa sababu simu yako inalandanishwa na akaunti kadhaa mtandaoni, huenda ukaona maingizo kadhaa ya anwani moja. Unaweza kuunganisha maelezo yote tofauti ya anwani kwenye ingizo moja katika orodha ya anwani.

1. Gusa **>** **> Anwani > ZOTE**.
2. Gusa na ushikilie ingizo la anwani, na kisha uchague anwani unazotaka kuunganisha.
3. Gusa **> Unganisha**.
4. Gusa **UNGANISHA** ili uthibitishe. Unaweza kurudia hatua hizi kuunganisha anwani nyingine.

# Akaunti za wavuti

## Kuongeza au kuondoa akaunti

Unaweza kuongeza akaunti kadhaa za Google na akaunti za Microsoft Exchange ActiveSync®. Pia unaweza kuongeza aina zingine za akaunti kulingana na programu zilizosakinishwa kwenye simu yako.

### Ongeza akaunti

1. Gusa ⬤ > ⠿ > **Mipangilio** > **Akaunti** > **Ongeza akaunti**.
2. Gusa aina ya akaunti unayotaka kuongeza.
3. Fuata hatua zilizo kwenye skirni kuingiza maelezo kuhusu akaunti. Akaunti nyingi zinahitaji jina la mtumiaji na nenosiri, lakini huenda maelezo yakatofautiana. Huenda pia ukahitaji taarifa fulani kutoka kwa usaidizi wa IT au msimamizi wako wa mfumo.

Wakati akaunti imeongezwa kwa mafanikio, inaonyeshwa katika menyu ya **Akaunti**.

### Ondoa akaunti

Kuondoa akaunti kutaifuta na maelezo yote yanayohusiana nayo kutoka kwenye simu yako, kama vile barua pepe na anwani.

1. Gusa ⬤ > ⠿ > **Mipangilio** > **Akaunti**.
2. Gusa kategoria ya akaunti na kishe uguse akaunti hiyo.
3. Gusa ⋮ > **Ondoa akaunti** > **ONDOA AKAUNTI**.

## Kusanidi ulandanishaji wa akaunti

### Sanidi mpangilio wa ulandanishaji otomatiki

1. Gusa ⬤ > ⠿ > **Mipangilio** > **Akaunti**.
2. Gusa ⋮ na uteue au utengue **Landanisha data kiotomatiki**.
   - ▶ Wakati mlandanisho otomatiki umewashwa, mabadiliko unayofanya kwenye maelezo yaliyo

kwenye simu yako au kwenye wavuti yanalandanishwa pamoja kiotomatiki.

- Wakati mlandanisho otomatiki umezimwa, unahitaji kulandanisha mwenyewe ili ukusanye barua pepe, usasisho, na maelezo mengine ya hivi karibuni.

## Landanisha mwenyewe

1. Gusa > > **Mipangilio > Akaunti**.
2. Gusa kategoria ya akaunti na kisha akaunti unayotaka kulandanisha.
3. Gusa > **Landanisha sasa hivi**. Au gusa aina za maelezo unayotaka kulandanisha.

## Badilisha mipangilio ya ulandanishaji ya akaunti

1. Gusa > > **Mipangilio > Akaunti**.
2. Gusa kategoria ya akaunti na kisha akaunti hiyo. Skrini ya **Ulandanishaji** inatokea, ikionyesha orodha ya maelezo ambayo akaunti yako inaweza kulandanisha.
3. Wakati ulandanishaji otomatiki umewezeshwa, washa au zima vipengele unavyohitaji. Aina za maelezo yaliyowezeshwa kwenye simu na wavuti zitawekwa katika ulandanishaji otomatiki. Wakati ulandanishaji otomatiki umelemazwa, gusa kipengele ulandanishe aina hiyo ya maelezo kati ya simu na wavuti.

# Barua pepe

Gusa katika skrini ya mwanzo na uchague **Barua pepe**. Itumie kupokea na kutuma barua pepe kutoka kwenye akaunti yako ya barua pepe ya tovuti au akaunti zingine, kutumia POP3 au IMAP, au kufikia akaunti yako ya Exchange ActiveSync kwa mahitaji yako ya barua pepe ya shirika.

## Kuunda akaunti ya kwanza ya barua pepe

1. Unapofungua **Barua pepe** kwa mara ya kwanza, ingiza anwani yako ya barua pepe na uguse **INAYOFUATA**.

   **DOKEZO:**

   Gusa **USANIDI WA KUFANYA MWENYEWE** ikiwa unataka kuingiza maelezo haya mwenyewe.

2. Ingiza nenosiri lako na uguse **INAYOFUATA**. Simu yako itaepua paramita za mtandao kiotomatiki.
3. Fuata maelekezo yaliyo kwenye skrini kukamilisha usanidi.

Simu yako itaonyesha kisanduku pokezi cha akaunti ya barua pepe na kuanza kupakua ujumbe wa barua pepe.

## Kuangalia barua pepe

Simu yako inaweza kuangalia barua pepe kiotomatiki kwa kipindi unachoweka wakati unaunda akaunti.

Pia unaweza kuangalia barua pepe mpya mwenyewe kwa kukokota orodha ya ujumbe chini.

## Kujibu simu

Unaweza kujibu au kusambaza ujumbe unaopokea. Pia unaweza kufuta ujumbe na kuudhibiti kwa namna zingine.

### Jibu au sambaza barua pepe

1. Fungua barua pepe unayotaka kujibu au kusambaza kutoka kwenye kisanduku pokezi.
2. Fanya yafuatayo kulingana na mahitaji yako:

   - Kumjibu mtu aliyekutumia barua pepe, gusa .

- Kumjibu mtu aliyekutumia barua pepe na wapokeaji wote wa barua pepe ya kwanza, gusa au > **Jibu kwa wote**.
- Kusambaza barua pepe kwa mtu mwingine, gusa au > **Sambaza**.

3. Hariri ujumbe wako na uguse .

### Weka barua pepe kama ambayo haijasomwa

Unaweza kurejeshe hali ya barua pepe iliyosomwa ionekana kama arua pepe ambayo haijasomwa - kwa mfano, ili ujikumbushe kuisoma tena baadaye. Pia unaweza kualamisha kundi la barua pepe kama barua ambazo hazijasomwa.

- Wakati unasoma ujumbe, gusa .
- Ukiwa katika orodha ya ujumbe (kwa mfano, kisanduku pokezi), gusa picha za mtumaji kando ya ujumbe na kisha uguse .

### Futa barua pepe

Unaweza kufuta barua pepe kutoka kwenye folda yake. Pia unaweza kufuta kundi la barua pepe.

- Wakati unasoma ujumbe, gusa .
- Ukiwa katika orodha ya ujumbe (kwa mfano, kisanduku pokezi), telezesha ujumbe kushoto au kulia ili uufute, au gusa picha za mtumaji kando ya ujumbe na kisha uguse .

**DOKEZO:**

Ukifuta ujumbe kwa bahati mbaya, gusa **Tengua** uuepue.

## Kuandika na kutuma barua pepe

1. Fungua kisanduku chako pokezi cha barua pepe na uguse .

   **DOKEZO:**

   Ikiwa una zaidi ya akaunti moja ya barua pepe kwenye simu, gusa mstari wa mtumaji uchague akaunti unayotaka kutumia kutuma ujumbe.

2. Ingiza jina au anwani ya barua pepe ya mpokeaji katika kipengele cha **Kwa**. Tenganisha kila mpokeaji kwa kutumia koma. Unaweza pia kugusa uongeze wapokeaji kutoka kwenye anwani zako.

   **DOKEZO:**

   Kutuma nakala au nakala fiche kwa wapokeaji wengine, gusa **> Ongeza Nkl/Nklf** ili ufungue kipengele cha **Nkl/Nklf** na uingize majina au anwani za barua pepe za wapokeaji.

3. Ingiza mada ya barua pepe na utunge ujumbe wa barua pepe.
4. Gusa ili uongeze faili za sauti, picha, video na aina zingine za faili kama viambatisho.
5. Gusa iliyo pande wa juu kulia mwa skrini ili utume ujumbe.

# Kuongeza na kuhariri akaunti za barua pepe

## Ongeza akaunti ya barua pepe

Baada ya kuunda akaunti yako ya kwanza ya barua pepe (angalia Kuunda akaunti ya kwanza ya barua pepe), unaweza kuongeza akaunti zaidi za barua pepe na kuzidhibiti zikiwa tofauti.

1. Fungua **Barua pepe** ili upate skrini ya kisanduku-pokezi.
2. Gusa **> Mipangilio > Ongeza akaunti**.
3. Fuata maelekezo ya kuunda akaunti kama ulivyofanya na akaunti ya kwanza.

## Hariri akaunti ya barua pepe

Unaweza kubadilisha idadi ya mipangilio ya akaunti, ikijumuisha marudio ya kuangalia barua pepe, unavyoarifiwa kuhusu barua pepe mpya, sahihi yako ya barua pepe, na maelezo zaidi kuhusu seva ambazo akaunti yako inatumia kutuma na kupokea barua pepe.

1. Fungua **Barua pepe** ili upate skrini ya kisanduku-pokezi.
2. Gusa **> Mipangilio** na uguse akaunti unayotaka kubadilisha mipangilio yake.
3. Fanya mabadiliko na uguse unapomaliza.

## Kubadilisha mipangilio ya jumla ya barua pepe

Mipangilio ya jumla inatumika kwenye akaunti zote za barua pepe unazoongeza.

1. Fungua **Barua pepe** ili upate skrini ya kisanduku-pokezi.
2. Gusa ☰ **> Mipangilio > Mipangilio ya jumla**.
3. Fanya mabadiliko na uguse ← unapomaliza.

# Ujumbe

Unaweza kutumia Ujumbe kutuma na kupokea ujumbe mfupi (SMS) na ujumbe wa medianuwai (MMS).

## Kufungua skrini ya ujumbe

Gusa > .

Skrini ya **Ujumbe** inafunguka, mahali unapoweza kutunga ujumbe mpya, kutafuta ujumbe, au kufungua mtungo wa ujumbe wa mawasiliano yanayoendelea.

- Gusa ili utunge ujumbe mpya mfupi au ujumbe wa medianuwai.
- Gusa ili utafute ujumbe ukitumia maneno msingi.
- Gusa ili utazama ujumbe wako wote, ujumbe ambao bado hujausoma, ujumbe unaoupenda zaidi, au matangazo ya kifaa rununu.
- Gusa mfumo uliopo wa ujumbe ili ufungue mazungumzo kati yako na nambari fulani.

## Kutuma ujumbe

1. Ukiwa kwenye skrini ya **Ujumbe**, gusa iliyo kwenye kona ya chini kulia.
2. Ongeza wapokeaji kwa njia moja kati ya zinazofuata.
   - Gusa kipengele cha **Kwa** na uingize nambari ya mpokeaji au jina la anwani mwenyewe. Ikiwa simu inatoa mapendekezo machache ya anwani, gusa anwani moja unayotaka kuiongeza.
   - Chagua wapokeaji kutoka kwenye anwani zako au nambari unazowasiliana nazo mara nyingi kwa kugusa .
3. Gusa kipengele cha **Aina ya ujumbe** na uandike ujumbe mfupi.

   Ikiwa unataka kutuma ujumbe wa medianuwai, gusa ili uongeze picha, sauti, video au aina nyingine ya faili kwenye ujumbe.

4. Gusa . Ikiwa kadi mbili ndogo za SIM zimesakinishwa, gusa au .

## Kujibu ujumbe

Ujumbe unaopokea unaambatishwa kwenye mitungo iliyopo ya nambari hiyo. Ikiwa ujumbe mpya unaingia kutoka nambari mpya, mtungo mpya unaundwa.

1. Kwenye skrini ya **Ujumbe**, gusa mtungo ulio na ujumbe unaotaka kujibu.
2. Andika jibu lako kwenye kisanduku cha ujumbe kilicho hapo chini au uguse ili utume picha, sauti, video au aina zingine za faili kwenye ujumbe huo.
3. Gusa . Ikiwa kadi mbili ndogo za SIM zimesakinishwa, gusa au .

## Kusambaza ujumbe

1. Kwenye skrini ya **Ujumbe**, gusa mtungo ulio na ujumbe unaotaka kusambaza.
2. Gusa na ushikilie ujumbe na kisha uguse **Sambaza** katika menyu inayofunguka.
3. Ingiza mpokeaji wa ujumbe na uhariri maudhui ikiwa unataka.
4. Gusa . Ikiwa kadi mbili ndogo za SIM zimesakinishwa, gusa au .

# Kivinjari wavuti

Tumia **Chrome** kutazama kurasa za wavuti na kutafuta maelezo.

## Kufungua kivinjari

Gusa > uzindue kivinjari wavuti.

Chrome pia hufunguka unapogusa kiungo cha wavuti - kwa mfano, katika barua pepe au ujumbe mfupi.

Kufungua ukurasa wa wavuti au kutafuta kwenye wavuti:

1. Fungua programu ya **Chrome**.
2. Gusa kisanduku cha anwani kilicho juu mwa ukurasa wa wavuti.
3. Ingiza anwani (URL) ua ukurasa wa wavuti au ingiza maneno unayotaka kutafuta.
4. Gusa URL au mapendekezo ya utafutaji au gusa kibonye cha ingiza kwenye kibodi iliufungue ukurasa wa wavuti au matokeo ya utafutaji.

## Kutumia vichupo vingi vya kivinjari

Unaweza kufungua kurasa kadhaa za wavuti kwa wakati mmoja (ukurasa mmoja katika kila kichupo) na ubadili kati ya vichupo hivyo kwa urahisi.

**Kufungua kichupo kipya cha kivinjari:**

Gusa > **Kichupo kipya**. Kichupo kipya cha kivinjari kinafunguka.

**Kubadili kati ya vichupo:**

1. Gusa ikoni ya 2 upande wa juu kulia mwa skrini. Idadi ya vichupo inaonyesha idadi ya sasa ya madirisha wazi ya kivinjari.
2. Telezesha wima ili ubiringize orodha ya vichupo vilivyofunguliwa.
3. Gusa kijipicha cha kichupo unachotaka kufungua.

**DOKEZO:**

Telezesha kijipicha upande wa mlalo au uguse yake ufunge kichupo.

## Kupakua faili

1. Gusa na ushikilie picha au kiungo cha faili au cha ukurasa mwingine wa wavuti.
2. Katika menyu inayofunguka, gusa **Pakua picha** au **Pakua kiungo**.

Faili zilizopakuliwa zimehifadhiwa kwenye simu yako. Unaweza kuzitazama au kuzifungua katika programu ya **Upakuzi**.

## Kubadilisha mipangilio ya Chrome

Unaweza kusanidi idadi ya mipangilio kukaidisha unavyovinjari wavuti, ikiwa ni pamoja na mipangilio kadhaa unayoweza kutumia kudhibiti faragha yako.

Kufungua skrini ya mipangilio ya Chrome, gusa ⋮ > **Mipangilio**.

# Kamera

Unaweza kutumia simu yako kupiga picha na kurekodi video. Picha na video zinahifadhiwa kwenye kadi ya microSD uliyosakinisha au katika hifadhi ya simu. Unaweza kuzinakili kwenye kompyuta yako au uzifikie katika programu ya **Picha**.

## Kupiga picha

1. Gusa  > .
2. Lenga kamera kwenye kitu unachotaka kupiga picha na ufanye marekebisho yoyote muhimu. PICHA (kamera otomatiki) hutumika kama kamera ya chaguo-msingi.




| Nambari | Kazi |
|---|---|
| 1 | Washa au zima kipengele cha HDR, kinapatikana kwa kamera ya nyuma peke yake. |
| 2 | Badilisha mipangilio ya kamera. |
| 3 | Geuza kwa modi ya PICHA. |

| Nambari | Kazi |
|---|---|
| 4 | Piga picha. |
| 5 | Tazama picha na video ulizopiga. |
| 6 | Geuza kwa modi ya KUFANYA MWENYWE, MFIDUO ANUWAI, au MUDA ULIOPITA. |
| 7 | Chagua matokeo ya rangi au matokeo mengine maalum. |
| 8 | Geuza kati ya kamera ya mbele na nyuma. |
| 9 | Geuza kwa modi ya VIDEO. |
| 10 | Badilisha mpangilio wa mwako, unapatikana kwa kamera ya nyuma peke yake. |
| 11 | Weka muda wa kusubiri kabla ya kamera kupiga picha kiotomatiki baada ya kugusa ikoni ya kilango. |

**ONYO!**

Kaa mbali kutosha wakati unatumia mwako. Usilenge mwako kwenye macho ya watu au wanyama.

**DOKEZO:**

Unaweza kupanua au kuchuna kwenye skrini ili ukuze au ufifize kabla ya kupiga picha.

3. Gusa kwa wepesi.

## Kurekodi video

Unaweza kurekodi klipu za video za kasi ya kawaida. Kamera ya nyuma pia hukuruhusu kurekodi video ya muda wa kusubiri.

1. Gusa > .
2. Gusa **VIDEO** ikiwa unataka kunasa video ya kasi ya kawaida. Kunasa video ya muda wa kusubiri, gusa **> MUDA WA KUSUBIRI**.
3. Lenga kamera kwenye kituo unachonasa kwenye video.

**DOKEZO:**

Unaweza kupanua au kuchuna kwenye skrini ili ukuze au ufifize kabla na wakati wa kurekodi.

4. Anza kurekodi.

▶ Katika hali ya **VIDEO**, gusa ili uanze kurekodi klipu ya video ya kasi ya kawaida.

▶ Katika modi ya **MUDA WA KUSUBIRI**, gusa ili urekodi video ya muda wa kusubiri.

**DOKEZO:**

Wakati unarekodi video ya kasi ya kawaida au muda wa kusubiri, gusa ili uhifadhi fremu kama picha tofauti.

5. Wacha kurekodi.

▶ Katika modi ya **VIDEO**, gusa .

▶ Katika modi ya **MUDA WA KUSUBIRI**, gusa .

## Kutumia modi ya kamera ya kufanya mwenyewe

Unaweza kutumia modi ya kamera ya kufanya mwenyewe kurekebisha chaguo zaidi za kamera kwa picha yako kama vile ISO, usawa wa weupe, mfiduo, nk.

1. Gusa > .
2. Gusa > **KUFANYA MWENYEWE**.
3. Lenga kamera kwenye kitu unachotaka kupiga picha na unaweza kufanya marekebisho yanayofuata.

▶ Kokota kisanduku cha manjano kwenye sehemu yoyote kwenye skrini unayotaka kamera kupima mfiduo ili urekebishe uangavu wa picha. Gusa na ushikilie kisanduku hicho ili ufunge mfiduo.

▶ Gusa ili ukunjue chaguo, ikiwa ni pamoja na ISO, mfiduo kamili, usawa wa weupe, na vipindi vya picha za muda wa kusubiri.

4. Gusa ikoni ya kilango ili upige picha.

# Muziki

Programu ya **Cheza Muziki** hufanya kazi na Muziki wa Google, duka la muziki la mtandaoni la Google na huduma za kutiririsha muziki. Unaweza kutiririsha muziki kupitia data rununu au Wi-Fi na usikilize nyimbo uzipendazo ulizoongeza kwenye maktaba ya Muziki wa Google ya mtandaoni. Unaweza pia kucheza faili za sauti ulizonakili moja kwa moja kwenye simu yako kutoka kwa kompyuta.

**DOKEZO:**


Upatikanaji wa Muziki wa Google unategemea eneo ulipo. Ikiwa haupatikani, au huna data rununu au muunganisho wa Wi-Fi, unaweza kucheza muziki uliohifadhiwa kwenye simu yako peke yake.

## Kucheza muziki wako

Gusa > > **Cheza Muziki**. Ukiagizwa, chagua akaunti ili ufikie maktaba yake ya muziki ya mtandaoni.

Programu hutafuta maktaba yako ya mtandaoni na simu yako kwa muziki na orodha za kucheza kabla ya kuonyesha maktaba yako ya muziki ya pamoja. Unaweza kugusa > **Maktaba ya muziki** ili uone muziki wote na orodha zote za kucheza. Kubadilisha mionekano ya maktaba yako, telezesha kushoto au kulia.

Gusa wimbo ili uucheze. Wakati wimbo unacheza, gusa maelezo ya ufupisho yaliyo hapo chini ili ionyeshe skrini ya kucheza.




| Nambari | Kazi |
|---|---|
| 1 | Maelezo ya wimbo na msanii. Gusa na ukokote chini ili urudi kwenye maktaba ya muziki. |
| 2 | Sanaa ya albamu (ikiwa ipo). Telezesha kushoto/kulia ili uende kwenye wimbo wa awali/unaofuata katika orodha ya kucheza. |
| 3 | Geuza modi ya kucheza. Unaweza kurudia wimbo wa sasa, urudie orodha ya kucheza ya sasa, au uzime urudiaji. |
| 4 | Kokota mwambaa wa maendeleo ili uruke kwenye sehemu nyingine ya wimbo |
| 5 | Onyesha unaupenda wimbo kwa kuweka kidole juu. |
| 6 | Udhibiti wa kucheza. Ruka nyimbo, au simamisha na uendelee kucheza. |
| 7 | Onyesha huupendi wimbo kwa kuweka kidole chini. |
| 8 | Washa au zima uchanganyaji. |
| 9 | Gusa ili uone orodha ya kucheza ya sasa (foleni). |
| 10 | Pata chaguo zaidi. |

Bado unaweza kudhibiti muziki wakati hauko katika skrini ya kucheza.

- Katika maktaba ya muziki ya programu ya **Cheza Muziki**, gusa taarifa ya ufupisho iliyo chini mwa skirni ili urejeshe skrini ya kucheza.
- Katika programu zingine, vuta paneli ya taarifa chini. Gusa jina la wimbo ili urejeshe skrini ya kucheza, au gusa au cheza wimbo wa awali au unaofuata. Gusa ili ucheze wimbo wa sasa, na uguse ili uusimamishe.
- Wakati skrini imefungwa, maelezo ya wimbo, jarida la albamu pamoja na udhibiti wa kucheza unaonyeshwa kwenye skrini. Unaweza kusimamisha/kuendelea kucheza au kuruka nyimbo.

## Kudhibiti orodha za kucheza

Unda orodha za kucheza ili upange faili zako za muziki kwa vikundi vya nyimbo, ili uweze kucheza nyimbo unazopenda kwa mpangilio unaopendelea.

**Kuunda orodha ya kucheza au kuongeza wimbo kwenye orodha ya kucheza:**

- Gusa iliyo kando ya wimbo na uchague **Ongeza kwenye orodha ya kucheza**. Gusa orodha ya kucheza uongeze wimbo.
- Gusa iliyo kando ya wimbo na uchague **Ongeza kwenye orodha ya kucheza**. Gusa **ORODHA MPYA YA KUCHEZA** uunde orodha mpya ya kucheza. Andika jina na ufafanuzi ili uhariri orodha ya kucheza, na uguse **UNDA ORODHA YA KUCHEZA.**

**Kuondoa wimbo kutoka orodha ya kucheza:**

1. Gusa **> Maktaba ya muziki** katika programu ya **Cheza Muziki**.
2. Gusa kichupo cha **ORODHA ZA KUCHEZA**, na uguse orodha ya kucheza.
3. Gusa iliyo kando ya wimbo katika orodha ya kucheza.
4. Gusa **Ondoa kutoka kwenye orodha ya kucheza**.

**Kufuta orodha ya kucheza:**

1. Gusa  **> Maktaba ya muziki** katika programu ya **Cheza Muziki**.
2. Gusa kichupo cha **ORODHA ZA KUCHEZA**.
3. Gusa  iliyo kandi ya orodha ya kucheza unayotaka kufuta.
4. Gusa **Futa > SAWA**.

**DOKEZO:**

Orodha za kucheza zilizoundwa kiotomatiki, kama vile **Vidole juu** na **Ya mwisho kuongezwa**, haziwezi kufutwa.

# Mipangilio

Gusa ⬤ > ⋯ > **Mipangilio**. Programu ya **Mipangilio** ina zana nyingi za kukaidisha na kusanidi simu yako.

Juu mwa skrini ya Mipangilio, unaweza kuona mapendekezo ya mpangilio. Gusa ili ukague au ukaidishe mipangilio inayopendekezwa.

## Pasi waya na mitandao

### Wi-Fi

Gusa ⬤ > ⋯ > **Mipangilio > Wi-Fi**. Unaweza kuwasha au kuzima Wi-Fi, na kusanidi miunganisho yako ya Wi-Fi. Angalia Kuunganisha kwenye Wi-Fi.

Wakati Wi-Fi imewashwa, gusa ⋮ > **Mahiri > Wi-Fi Direct** katika menyu ya **Wi-Fi** kushiriki data kati ya vifaa viwili moja kwa moja kupitia Wi-Fi. Angalia Unganisha kwenye kifaa kingine kupitia Wi-Fi Direct.

### Bluetooth

Gusa ⬤ > ⋯ > **Mipangilio > Bluetooth**. Unaweza kuwasha au kuzima Bluetooth, na kusanidi miunganisho yako ya Bluetooth. Angalia Kuunganisha kwenye vifaa vya Bluetooth.

### Kadi za SIM

Gusa ⬤ > ⋯ > **Mipangilio > Kadi za SIM** ili udhibiti matumizi ya kadi mbili za SIM. Unaweza kuwezesha au kulemaza kadi ndogo za simu zilizoingizwa, kuzima au kuwasha data rununu, kubadilisha majina na rangi ya kadi, au kuchagua kadi unayotaka kutumia kwa data, simu, au ujumbe. Angalia Dhibiti matumizi ya SIM mbili.

### Matumizi ya data

Gusa ⬤ > ⋯ > **Mipangilio > Matumizi ya data** ili ukague na kudhibiti matumizi ya data rununu. Unaweza kutazama na kuzuia matumizi ya data ya Wi-Fi pia.

- Guda **Kihifadhi Data** ili uwezeshe Kihifadhi data kinachozuia programu kutumia muunganisho wa data chinichini. Kwa programu unayotumia kwa sasa, inaweza kufikia data, lakini inaweza kufanya hivyo mara chache wakati Kihifadhi Data kimewezeshwa. Pia unaweza kugusa **Ufikiaji wa data usiozuiwa** na uruhusu baadhi ya programu kufikia muunganisho wa data hata wakati Kihifadhi data kimewashwa.
- Gusa swichi ya **Data rununu** ili uzime au uwashe data rununu.
- Gusa **Matumizi ya data rununu** ili ukague kiasi cha data kilichotumika wakati wa kipindi cha muda ulioweka, angalia programu ambazo zimekuwa zikitumia data rununu, zuia data ya chinichini kwa programu kibinafsi, au ruhusu matumizi ya data yasiyozuiwa wakati Kihifadhi data kimewashwa.
- Gusa **Kipindi cha bili** ili uweke tarehe ya kuweka upya kipindi cha matumizi ya data, na uweke onyo na kikomo cha data rununu.
- Gusa **Matummizi ya data ya Wi-Fi** ili utazame matumizi ya Wi-Fi ya programu.
- Gusa **Vizuizi vya mtandao** ili uchague mitandao ya Wi-Fi ambayo ni Wi-Fi rununu. Programu huenda zikakuonya kabla ya kutumia mitandao hii kwa upakuzi mikubwa ili kuepkua bili kubwa za data rununu.

DOKEZO:

Matumizi ya data hupimwa na simu yako, na hesabu la matumizi ya data ya mtoa huduma wako huenda likawa tofauti.

## Modi ya ndege

Gusa > > **Mipangilio > Zaidi** na utelezeshe swichi iliyo kando ya **Modi ya ndege** ili uwashe au uzime modi ya ndege. Redio zote za simu zinazotangaza sauti au data zinazimwa wakati modi ya ndege imewashwa.

## Wavuti wa kuunganisha na kubebeka

Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > Wavuti wa kuunganisha na kubebeka** ili ushiriki muunganisho wa data rununu wa simu yako na kompyuta au vifaa vingine kupitia USB, Bluetooth au Wi-Fi. Angalia Kushiriki muunganisho wako wa data rununu.

## VPN

Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > VPN** ili uuenda na kuunganisha kwenye mitandao mnemba ya kibinafsi. Angalia Kuunganisha kwenye mitandao mnemba ya kibinafsi.

## Mitandoa rununu

Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > Mitandao rununu** ili udhibiti utambizi wa data rununu, uweke aina ya mtandao, uweke majina ya eneo la ufikiaji na uchague mtandao rununu, nk. Angalia Kuunganisha kwenye mitandao rununu.

## Uwekaji upya wa mipangilio ya mtandao

Gusa > > **Mipangilio > Zaidi > Uwekaji mpya wa mipangilio ya mtandao** ili uweke mipangilio yote ya mtandao, ikiwa ni pamoja na Wi-Fi, data rununu, na mipangilio ya Bluetooth.

# Kifaa

## Onyesho

Gusa > > **Mipangilio > Onyesho** ili usanidi chaguo zinazofuata.

- **Paneli ya programu unazozipenda zaidi:** Wakati kipengele hiki kimewezeshwa, unaweza kutelezesha kulia kwenye skrini ya mwanzo ya kushoto kabisa ili ufungue programu ulizoweka kama unazozipenda zaidi.
- **Programu unazozipenda zaidi za kwenye skrini ya mwanzo:** Chagua programu zinazofunguka unapotelezesha kulia kwenye skrini ya mwanzo ya kushoto kabisa.
- **Funga mpangilio wa skrini ya mwanzo:** Washa ili uzuie mabadiliko yoyote ya skrini ya mwanzo.
- **Vitufe vya urambazaji:** Kokota vitufe vya urambazaji vilivyo chini mwa skrini ili uvipange upya.
- **Mikato ya skrini iliyofungwa:** Onyesha ikoni za mikato kwenye skrini iliyofungwa. Unaweza kutelezesha kutoka kwenye ikoni ya mkato iliyo upande wa chini wa skrini ili ufungue programu au kipengele husika.

- **Hariri mikato ya skrini iliyofungwa:** Gusa mkato wa skrini iliyofungwa ili uibadilishe au uiondoe, au gusa **Ongeza mkato** ili uongeze mkato.
- **Kiwango cha uangavu:** Weka uangavu wa onyesho.
- **Uangavu zoefu:** Sawazisha uangavu wa skrini kiotomatiki.
- **Jina la opareta wa mtandao:** Onyesha jina la opareta wa mtandao kushoto mwa mwambaa wa hali.
- **Asilimia ya nishati ya betri:** Onyesha au ficha asilimia ya nishati ya betri: katika mwambaa wa hali.
- **Pazia:** Chagua picha au uhuishaji wa mandhari-nyuma wa skrini ya mwanzo na skrini iliyofungwa.
- **Lala:** Weka muda wa kutotumika kabla ya skrini kuzima kiotomatiki.
- **Gusa mara mbili uiwashe:** Gusa skrini mara mbili ili uiwashe wakati simu iko katika modi ya kulala.
- **Kilezi:** Dhibiti kipengele cha kilezi. Kikiwezeshwa, saa, rangi, habari na hali ya hewa, au picha zitaonyesha kama kilezi.
- **Mwamba wa taarifa wa kupepesa:** Hupepesa mwangaza wa ishara kukujulisha kuhusu simu ulizokosa, ujumbe mpya, na matukio mengine.
- **Ukubwa wa fonti:** Weka ukubwa wa fonti wa maandishi yaliyo kwenye skrini.
- **Ukubwa wa onyesho:** Sawazisha ukubwa wa onyesho wa vipengele vinavyojumuisha fonti, ikoni na picha kwenye skrini.
- **Wakati kifaa kinazungushwa:** Chagua kama maudhui ya skrini yanafaa kuzunguka wakati simu inazungushwa.

## Taarifa

Gusa > **> Mipangilio > Taarifa**. Unaweza kuweka chaguo tofauti za taarifa kwa programu binafsi. Gusa programu ili uzuie au unyamazishe taarifa, uchague maudhui ya taarifa zake ya kuonyesha kwenye skrini ya kufunga, au uruhusu taarifa zake kuandikiza kwenye mipangilio yako ya Usinisumbue.

## Sauti

Gusa > > **Mipangilio > Sauti**. Unaweza kusawazisha aina tofauti za viwango-sauti, uweke chaguo za Usinisumbue, uweke milio ya simu, taarifa, na ving'ora, usanidi matangazo ya dharura, na uchague sauti za mfumo.

## Programu

Gusa > > **Mipangilio > Programu** ili uone programu zilizosakinishwa kwenye simu yako na uzidhibiti.

Gusa programu ili uone maelezo yake. Chaguo zinazofuata huenda zikapatikana:

- **SIMAMISHA KWA LAZIMA:** Simamisha programu.
- **SAKINUSHA:** Sakinusha programu.
- **LEMAZA/WEZESHA**: Lemaza au wezesha programu.
- **Hifadhi:** Kagua maelezo yake ya hifadhi, futa data au kache yake.
- **Matumizi ya data:** Kagua kiasi cha data kilichotumiwa na programu wakati wa kipindi cha muda ulichoweka na uzuie data ya chinichini ya programu.
- **Ruhusa:** Kagua na ubadilishe ruhusa za programu.
- **Taarifa:** Weka chaguo za taarifa za programu.
- **Fungua kwa chaguo-msingi:** Kagua viungo vinavyokubaliwa na programu na uweke kama unataka vifunguliwe katika programu, na ufute chaguo-msingi za programu.
- **Betri:** Kagua maelezo ya matumizi ya betri ya programu tangu mara ya mwisho kuchajiwa kabisa.
- **Kumbukumbu:** Kagua kiasi cha kumbukumbu kilichotumiwa na programu.

**DOKEZO:**

Sio chaguo zote zinapatikana kwa programu. Baadhi ya programu zina chaguo zaidi.

## Programu chaguo-msingi

Gusa > > **Mipangilio > Programu chaguo-msingi** ili uweke chaguo zinazofuata.

- **Kufungua viungo:** Kagua viungo vinavyokubaliwa na programu na uweke kama unataka vifunguliwe katika programu, na ufute chaguo-msingi za programu.
- **Usaidizi wa ingizo na ingizo la sauti:** Chagua programu chaguo-msingi ya usaidizi wa sauti na ingizo, na uweke chaguo husika za programu.
- **Programu ya mwanzo/Programu ya kivinjari/Programu ya simu/Programu ya SMS:** Chagua programu chaguo-msingi ya kizinduzi, kuvinjari wavuti, kupiga simu na ujumbe.
- **Ufikiaji maalum:** Weka chaguo za ufikiaji maalum za programu.

## Hifadhi

Gusa > > **Mipangilio > Hifadhi** ili utazame maelezo ya kumbukumbu ya hifadhi ya ndani ya simu na kadi ya microSD.

Unaweza kuchagua mahali chaguo-msingi kwa data mpya, kama vile picha zinazopigwa na sauti zinazorekodiwa. Gusa **Mahali pa hifadhi** na uchague **Simu** au **Kadi ya SD** uhifadhi vitu katika hifadhi ya simu au kadi ya microSD iliyoingizwa.

Gusa **Hifadhi ya ndani inayoshirikishwa** ili upate maelezo kamili ya matumizi ya nafasi kulingana na aina. Gusa aina ya data ili uone maelezo zaidi au ufute faili ambazo huhitaji, au gusa **Vinjari** ili utazame na udhibiti faili zote zilizo katika hifadhi.

Kwa maelezo zaidi kuhusu hifadhi ya ndani na kadi ya microSD, angalia Kutumia kadi ya microSD kama hifadhi ya kubebeka au ya ndani.

## Kidhibiti nishati

Gusa > > **Mipangilio > Kidhibiti Nishati** kwa usimamizi wa nishati. Unaweza kutazama kiwango cha nishati cha betri, kukagua programu zilizotumia betri, kuchagua mpango unaofaa wa nishati na usadifishe matumizi ya betri, na zaidi.

## Kumbukumbu

Gusa > > **Mipangilio > Kumbukumbu** ili ufuatilie matumizi wastani ya kumbukumbu na utendaji wa simu yako. Pia unaweza kuangalia programu zinazotumia kumbukumbu kubwa.

## Watumiaji

Gusa > > **Mipangilio > Watumiaji** udhibiti akaunti za watumiaji wa simu yako.

Unaweza kushiriki simu yako na watu wengine kwa kuunda akaunti zaidi za watumiaji. Kila mtumiaji mwenye akaunti tofauti ana nafasi yake ya hifadhi, pazia, ufungaji wa skrini na zaidi. Watumiaji pia wanaweza kurekebisha mipangilio ya kifaa kama vile Wi-Fi inayoathiri kila mtu na kusasisha programu kwa watumiaji wote wengine.

Kwa chaguo-msingi, akaunti ya Mgeni inapatikana kwa kila mtu anayehitaji kutumia simu yako kwa muda mfupi. Unaweza kugusa **Ongeza mtumiaji** uunde akaunti zaidi za watumiaji.

Unaweza kugusa **Maelezo ya dharura** ili uunde maelezo na anwani zako za dharura. Maelezo unayoingiza yanaweza kusaidia timu ya huduma ya kwanza wakati wa dharura. Mtu yoyote anaweza kuyasoma kutoka kwenye kidayo cha dharura bila kufungua simu yako.

**VIDOKEZO:**

- Gusa kilicho kando ya akaunti ili usanidi chaguo zake.
- Wakati mtumiaji mgeni anatumia simu yako, anaweza kugusa **Ondoa mgeni** katika menyu ya **Watumiaji** ili afute data yake yote kutoka kwenye simu yako.

# Maelezo ya kibinafsi

## Eneo

Gusa > > **Mipangilio > Eneo** ili udhibiti huduma za eneo, zinazosaidia simu na programu yako kujua eneo lako. Ili utumie programu zinazotumia eneo, kama vile kutafuta eneo lako kwenye Ramani za Google, lazima uwe umewezesha huduma za eneo kwenye simu yako.

1. Telezesha swichi iliyo upande wa juu kulia ili uwashe au uzime huduma za eneo.
2. Wakati eneo limewezeshwa, gusa **Modi** ili uchague vyanzo vya eneo unavyotaka kutumia. Ili upate eneo lako sahihi, chagua **Usahihi wa juu**. Kuhifadhi nishati ya betri na kupata eneo la karibu, chagua **Kuhifadhi betri**. Kutumia GPS peke yake kutafuta eneo lako, chagua **Kifaa peke yake**.

## Usalama

Gusa  >  > **Mipangilio > Usalama** ili usanidi chaguo zinazosaidia kulinda simu na data yako.

- **Ufungaji wa skrini:** Lemaza ufungaji wa skrini au uuwezeshe kwa kutelezesha, mchoro, PIN, au nenosiri.

  Gusa  iliyo kando ya **Ufungaji wa skrini** ili uweke chaguo zinazofuata.

  - **Onyesha mchoro:** Onyesha mchoro unapouchora. Chaguo hii inapatikana wakati mchoro wa kufungua umewekwa.
  - **Funga kiotomatiki:** Weka muda unaohitajika kwa ufungaji kuamilishwa baada ya skrini kuzima. Chaguo hii inapatikana wakati mchoro wa kufungua, PIN au nenosiri limewekwa.
  - **Kitufe cha nishati kunafunga simu mara moja:** Ufungaji unaamilishwa mara moja baada ya kubonyeza kibonye cha **Nishati**. Chaguo hii inapatikana wakati mchoro wa kufungua, PIN au nenosiri limewekwa.
  - **Ujumbe wa skrini iliyofungwa:** Weka maandishi yanayoweza kuonyeshwa kwenye skrini iliyofungwa.

- **Ufungaji Mahiri:** Wacha simu yako ikiwa haijafungwa ikiwa unaamini iko salama. Ufungaji Mahiri unaweza kufanya hivi kwa kutambua kama simu yako iko mfukoni mwako au karibu na nyumbani mwako. Gusa  >  > **Mipangilio > Usalama > Ufungaji Mahiri > Utambuaji wa kuwa kwenye mwili** na utelezeshe kwenye swichi.

- **Fichamisha simu:** Gusa  >  > **Mipangilio > Usalama > Fichamisha simu** ili ufichamishe akaunti yako, mipangilio, programu zilizopakuliwa na data yake, media na faili zingine.

- **Weka ufungaji wa kadi ya SIM:**

  - **Funga kadi ya SIM:** Amilisha au amilishua ufungaji wa PIN ili mtumiaji ahitajike kuingiza PIN kabla ya kufikia kadi ndogo ya SIM.
  - **Badilisha PIN ya SIM:** Badilisha PIN inayotumiwa kufikia kadi ndogo ya SIM.

**DOKEZO:**

Weka manenosiri yako yote ya siri mahali salama kwa matumizi ya siku zijazo. Ukiingiza PIN ya SIM isiyo halali zaidi ya mara inayoruhusiwa, kadi yako ndogo ya SIM itafungwa na hutaweza kufikia mtandao wa simu rununu. Wasiliana na mtoa huduma wako kwa Ufunguo wa Kufungua PIN (PUK) ili urejeshe kadi ndogo ya SIM.

- **Onyesha manenosiri:** Onyesha manenosiri unapoyaingiza.
- **Wasimamizi wa kifaa:** Tazama au amilishua programu ulizoruhusu kuwa wasimamizi wa kifaa.
- **Vyanzo visivyojulikana:** Teua chaguo hii ili uruhusu usakinishaji wa programu kutoka vyanzo mbali na Play Store.
- **Aina ya hifadhi:** Kagua aina ya stakabadhi za hifadhi.
- **Stakabadhi zinazoaminika:** Onyesha vyeti vinavyoaminika vya CA.
- **Stakabadhi za mtumiaji:** Tazama na urekebishe stakabadhi zilizohifadhiwa.
- **Sakinisha kutoka kwenye kadi ya SD:** Sakinisha vyeti kutoka hifadhi ya ndani au kadi ya microSD.
- **Futa stakabadhi:** Futa vyeti vyote.
- **Wakala waaminifu:** Tazama au amilishua wakala waaminifu.
- **Ubanaji wa skrini:** Weka skrini unayotaka katika mtazamo, ili watu wengine wasiweze kubadilisha na programu zingine na kufikia maelezo yako ya kibinafsi. Gusa chaguo hii ili uone unavyofanya kazi.
- **Programu zilizo na ufikiaji wa matumizi:** Washa au zima baadhi ya programu za ufikiaji wa maelezo ya matumizi yako ya simu.

## Ruhusa za programu

Gusa > **> Mipangilio > Ruhusa za programu** ili uangalie ni programu gani zimeruhusiwa kufikia ruhusa fulani. Pia unaweza kubadilisha ruhusa za simu.

**ONYO!**

Kubadilisha ruhusa za programu kunaweza kusababisha programu kutofanya kazi vizuri au kama zilivyokusudiwa.

## Akaunti

Gusa ⚪ > ⚪ > **Mipangilio > Akaunti** ili udhibiti akaunti zako za mtandaoni na ulandanishaji. Gusa **Ongeza akaunti** ili uingie au uunde akaunti kwenye simu yako.

Gusa aina ya akaunti ili uone aina hizo za akaunti ulizoongeza na urekebishe mipangilio ya akaunti hizo.

## Google

Gusa ⚪ > ⚪ > **Mipangilio > Google** ili udhibiti mipangilio kwa urahisi kwa programu na vipengele vya Google. Unaweza kuweka chaguo za akaunti na huduma za Google.

## Lugha na ingizo

Gusa ⚪ > ⚪ > **Mipangilio > Lugha na ingizo** ili usanidi chaguo husika kwa lugha ya mfumo, mbinu za ingizo, ingizo na matokeo ya matamshi pamoja na ingizo la puku/padi.

- **Lugha:** Chagua lugha ya mfumo wako.
- **Kikagua tahajia:** Tumia Kikagua Tahajia cha Google ukague hitilafu za tahajia wakati unaingiza maandishi.
- **Kamusi ya kibinafsi:** Ongeza maneno mapya kwenye kamusi ya simu na uondoe maneno kutoka kwenye kamusi. Maneno unayoongeza hutumiwa kwa ukaguzi wa tahajia na mapendekezo ya maneno.
- **Kibodi na mbinu za ingizo:** Sanidi mipangilio ya ingizo la maandishi. Angalia Mipangilio ya mbinu za ingizo. Pia unaweza kuweka chaguo husika wakati kibodi halisi imeunganishwa kwenye simu.
- **Matokeo ya maandishi kwa matamshi:** Chagua injini ya kuunganisha matamshi au ubadilishe mipangilio yake, weka kiwango na mfinyo wa matamshi, cheza sampuli fupi ya kiunganishi cha matamshi, na ukague kama kipengele cha maandishi kwa matamshi kinakubali lugha ya mfumo ya sasa.
- **Kasi ya kidosa:** Chagua kasi ambayo kidosa/puko inafaa kubiringiza unapounganisha simu kwenye padi au kikorokoro cha puku.

### Akibisha na uweke upya

Gusa > > **Mipangilio > Akibisha na uweke upya** ili udhibiti chaguo za uakibishaji na urejeshaji wa data, na uweke mpangilio wa mtandao upya au simu kwa hali ya kiwanda.

- **Akibisha data yangu:** Akibisha data ya programu, manenosiri ya Wi-Fi, na mipangilio ingine kwenye seva za Google baada ya kuingia kwenye akaunti yako ya Google.
- **Akaunti ya akibisho:** Weka akaunti ya Google ambayo data inaakibishwa.
- **Rejesha kiotomatiki:** Rejesha mipangilio na data iliyoakibishwa hapo awali unaposakinisha programu upya.
- **Uwekaji upya wa data ya kiwanda:** Weka simu yako upya kwenye mipangilio ya chaguo-msingi ya kiwanda. Data yako yote iliyo katika hifadhi ya ndani itafutwa wakati wa uchakataji.

## Mfumo

### Tarehe na saa

Gusa > > **Mipangilio > Tarehe na saa** ili uweke tarehe, saa, kanda ya saa, na fomati ya saa. Pia unaweza kutumia data inayotolewa na mtandao.

### Uwashaji na uzimaji uliopangwa

Gusa > > **Mipangilio > Uwashaji na uzimaji uliopangwa** ili uweke siku na saa wakati simu inawaka au kuzima kiotomatiki. Pia unaweza kugusa swichi zilizo upande wa kulia ili uwashe au uzime vipengele.

### Ufikikaji

Gusa > > **Mipangilio > Ufikikaji** ili usanidi programu-jalizi na huduma za ufikikaji kwenye simu yako, kama vile **Ubadilikaji wa rangi au Ukubwa wa onyesho** kwa watumiaji wenye matatizo ya kuona.

## Uchapishaji

Gusa > > **Mipangilio > Uchapishaji** ili udhibiti huduma ya Google Cloud Print au programu zingine jalizi za printa zilizosakinishwa kutoka kwenye Google Play Store au mtengenezaji wa printa yako.

## Kuhusu simu

Gusa > > **Mipangilio > Kuhusu simu** ili uone maelezo muhimu ya simu na ya kisheria. Pia unaweza kugusa **Usasisho wa programu** upitie usasisho wa mfumo na uusakinishe unapopatikana.

# Usuluhishaji

Ukikumbana na matatizo wakati unatumia simu, au ikiwa haitafanya kazi ipasavyo, unaweza kupitia chati iliyo hapa chini. Ikiwa tatizo lako haliwezi kutatuliwa kwa kutumia maelezo yaliyo kwenye chati, wasiliana na mchuuzi uliponunua simu hiyo.

| **Tatizo** | **Sababu zinazowezekana** | **Suluhisho linalowezekana** |
|---|---|---|
| Mapokezi hafifu ya mawimbi | Mawimbi ya mtandao ni hafifu sana katika eneo ulipo, kwa mfano, katika sehemu ya chini ya nyumba au karibu na jengo refu, kwa sababu urushaji wa mawimbi pasi waya hauwezi kukufikia vizuri. | Nenda kwenye eneo ambapo wimbi la mtandao linaweza kupokewa vizuri. |
| | Mtandao unatumika kwa sasa (kwa mfano, wakati watu wengi hupiga simu, huenda kukawa na trafiki kubwa sana kwenye mtandao kuwezesha simu zaidi). | Jaribu usitumie simu wakati huo, au jaribu tena baada ya kusubiri kwa muda mfupi. |
| | Uko mbali sana na kituo cha mtoa huduma wako. | Unaweza kuagiza ramani ya huduma ya katika eneo ulipo kutoka mtoa huduma wako. |
| Mwangwi au kelele | Ubora wa kiungo cha mtandao ni hafifu upande wa mtoa huduma wako. | Kata simu na upige tena. Unaweza kuhamishwa kwenye kiungo bora zaidi cha mtandao au laini bora ya simu. |

| Tatizo | Sababu zinazowezekana | Suluhisho linalowezekana |
|---|---|---|
| | Ubora wa laini ya simu unayopigia simu uko chini. | Kata simu na upige tena. Unaweza kuhamishwa kwenye kiungo bora zaidi cha mtandao au laini bora ya simu. |
| Huwezi kuchagua vipengele fulani | Mtoa huduma wako haruhusu vipengeli hivi, au hujaomba huduma zinazotoa vipengele hivi. | Wasiliana na mtoa huduma wako. |
| Huwezi kuchaji betri | Betri au chaja ya betri imeharibika. | Wasiliana na mchuuzi. |
| | Halijoto ya simu iko chini ya 0 °C au zaidi ya 45 °C. | Rekebisha mazingira ya kuchaji betri ili uepuke hali joto kali zaidi. |
| | Mguso kati ya plagi ya kuchaji na chaja ni hafifu. | Kagua viunganishi vyote ili uhakikishe kwamba miunganisho yote iko sawa. |
| Muda mfupi wa kusubiri | Muda wa kusubiri unahusiana na usanidi wa mfumo wa mtoa huduma wako. Simu moja inayotumiwa na mifumo ya watoa huduma tofauti haitakuwa na urefu sawa wa muda wa kusubiri. | Ikiwa uko katika eneo ambapo wimbi ni hafifu, zima simu kwa muda mfupi. |
| | Betri limekwisha. Katika mazingira ya halijoto ya juu, maisha ya betri yatapungua. | Wasiliana na mchuuzi ubadilishe na betri lipya. |

| **Tatizo** | **Sababu zinazowezekana** | **Suluhisho linalowezekana** |
|---|---|---|
| | Ikiwa huwezi kuunganisha kwenye mtandao, simu itaendelea kutuma mawimbi ikijaribu kutafuta kituo cha mtoa huduma. Kufanya hivyo kunatumia nishati ya betri na hatimaye kutapunguza muda wa kusubiri. | Badilisha eneo lako uende mahali mtandao unafikika, au zima simu yako kwa muda. |
| Huwezi kuwasha simu yako | Nishati ya betri imekwisha. | Chaji betri la simu. |
| Hitilafu ya kadi ndogo ya SIM | Kasoro za kadi ndogo ya SIM au imeharibika. | Peleka kadi ndogo ya SIM kwa mtoa huduma wako ipimwe. |
| | Kadi ndogo ya SIM imeingizwa vibaya. | Ingiza kadi ndogo ya SIM vizuri. |
| | Kuna uchafu kwenye sehemu za mguso za kadi ndogo ya SIM. | Tumia kitambaa kisafi na kikavu kusafisha sehemu za mguso za kadi ndogo ya SIM. |
| Huwezi kuunganisha kwenye mtandao | Kadi ndogo ya SIM sio halali. | Wasiliana na mtoa huduma wako. |
| | Hauko karibu na eneo la huduma ya mtandao. | Hakikisha eneo la huduma kutoka kwa mtoa huduma wako. |
| | Wimbi ni hafifu. | Nenda mahali wazi, au ikiwa uko ndani ya jengo, hamia karibu na dirisha. |
| Huwezi kujibu simu zinazoingia | Umeamilisha kipengele cha **Kuzuia simu**. | Lemaza kipengele hiki. |

<table>
<tr><th>Tatizo</th><th>Sababu zinazowezekana</th><th>Suluhisho linalowezekana</th></tr>
<tr><td rowspan="2">Huwezi kupiga simu</td><td>Umeamilisha kipengele cha Kuzuia simu.</td><td>Lemaza kipengele hiki.</td></tr>
<tr><td>Umeamilisha kipengele cha Nambari za kudumu.</td><td>Lemaza kipengele hiki.</td></tr>
<tr><td>Msimbo wa PIN imezuiwa</td><td>Umeingiza msimbo wa PIN usio halali mara tatu mfululizo.</td><td>Wasiliana na mtoa huduma wako. Ikuwa mtoa huduma anakupa msimbo wa PUK wa kadi ndogo ya SIM, tumia msimbo huo wa PUK kufungua kadi ndogo ya SIM.</td></tr>
<tr><td rowspan="3">Simu inakwama, inajiwasha upya, au haiwezi kuwaka</td><td rowspan="3">Programu ya mshirika wa tatu sio tangamani na simu yako.</td><td>Sakinusha programu ambayo huenda ikawa inasabaisha tatizo hili.</td></tr>
<tr><td>Sasisha programu ya simu.</td></tr>
<tr><td>Weka simu kwenye hali ya kiwanda.</td></tr>
</table>

© Vodafone Group 2017. Vodafone, Vodacom na nembo ya Vodafone ni alama za biashara ya Vodafone Group. Bidhaa yoyote au majina ya kampuni yaliyotajwa humu ndani yanaweza kuwa alama ya biashara ya wamiliki wao husika.